
**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2020/2021

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHE. MMANGA MJENGO MJAWIRI (MBM) WAZIRI WA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI**

**MEI, 2020**



**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri (MBM)**
**Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar**

**YALIYOMO**

YALIYOMO .......... i
UTANGULIZI .......... 1
UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA .......... 3
HALI YA UZALISHAJI .......... 4
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020 .......... 8
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020 .......... 8
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2019/2020 .......... 10
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 .......... 19
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO .......... 19
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji .......... 20
Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo .......... 21
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo .......... 23
Programu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo .......... 24
Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe .......... 25
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA .......... 27
Programu Ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu .......... 27
Programu Ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka .......... 30
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO .......... 31
Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo .......... 31
Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo .......... 33
Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo .......... 34

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI .......... 35
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari .......... 36
Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini .......... 37
Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini .......... 39
Kampuni ya Uvuvi .......... 40
PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA .......... 42
Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara .......... 43
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji .......... 45
Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba .......... 47
CHANGAMOTO .......... 48
HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO .......... 50
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 .......... 53
MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKAWA FEDHA 2020/2021 .......... 53
MAKADIRIO YA MATUMIZI 2020/2021 .......... 53
MALENGO YA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 .......... 55
SHABAHA ZA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021 .......... 58
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO .......... 58
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Umwagiliaji Maji .......... 59
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo kwa Mwaka 2020/2021 .......... 61
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Kilimo Mwaka 2020/2021 .......... 62
Shabaha Zitakazotolewa na Wakala wa Serikali wa Huduma

za Matrekta na Zana za Kilimo kwa Mwaka 2020/2021 ......... 64
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa Mwaka 2020/2021 ......... 64
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA ......... 65
Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu kwa mwaka 2020/2021 ......... 66
Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka 2020/2021 ......... 67
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO ......... 68
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka 2020/2021 ......... 68
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo kwa Mwaka 2020/2021 ......... 69
Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ......... 70
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI ......... 71
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini ......... 72
Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini ......... 73
Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini ......... 74
Kampuni ya Uvuvi ......... 75
PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA UTAWALA WA KAZI ZA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI ... 76
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ......... 77
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ......... 78
Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Pemba ......... 78
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ......... 80
SHUKURANI ......... 81
VIAMBATANISHO ......... 84

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu kwa lengo la kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (PBB).

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia na kuibariki Zanzibar kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu ambapo asilimia kubwa wanajihusisha na kazi za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Uhifadhi wa Maliasili. Tunamuomba Mwenye Enzi Mungu mwingi wa rehma atupe shufaa na ayaondoshe maradhi haya ya KORONA nchini mwetu na duniani kote.

3. **Mheshimiwa Spika,** pongezi na shukurani za pekee zimuendee Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, usalama, amani na utulivu. Aidha, tunampongeza Mhe. Rais kwa kutoa miongozo na kusimamia vyema utekelezaji wa malengo ya ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka

2015 - 2020. Utekelezaji huu umeweza kufikia malengo yaliyowekwa kwa zaidi ya asilimia mia moja na mafanikio yaliyopatikana yameisaidia kwa kiasi kikubwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi sambamba na kuongeza tija kwa wananchi na kukuza uchumi.

**4.** **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa utendaji wake mkubwa ikiwa ni pamoja na kumsaidia na kumshauri vizuri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake jambo ambalo limeleta manufaa makubwa kwa wananchi hasa kupitia Sekta ya Kilimo. Vile vile, shukurani pia ziende kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwashauri vyema viongozi wetu na kufanya maamuzi mema na kutumia hekima na busara kubwa katika kuleta maendeleo na kulinda haki za wananchi wote.

**5.** **Mheshimiwa Spika,** nampongeza kwa dhati Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa umakini na umahiri wake wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaomsaidia kuliongoza Baraza na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

**6.** **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwakilishi wa Jimbo la Dimani pamoja na Wajumbe wote na Sekretarieti ya Kamati hiyo kwa miongozo na ushauri waliotoa kwa

Wizara ya Kilimo katika kufanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2019/2020. Vilevile, tunatanguliza shukurani za dhati kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kutupa michango na miongozo mizuri iliyotusaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/2021. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo tumeyazingatia katika ukamilishaji wa bajeti hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA

**7.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo ikijumuisha mazao, mifugo, uvuvi, misitu na maliasili zisizorejesheka bado inaendelea kuwa ni mhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar na inatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha ambapo asilimia 40 ya wananchi wameajiriwa na sekta hii; na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta ya kilimo katika kujikimu kimaisha. Sekta hii kwa mwaka 2019 imechangia asilimia 21.2 ya Pato la Taifa (mazao asilimia 7.4, mifugo 7.8, maliasili 1.2 na uvuvi 4.8 - OCGS 2019) na kuonesha kushuka ikilinganishwa na asilimia 21.3 mwaka 2018. Kushuka kwa uchangiaji wa sekta ya kilimo kumetokana na ukuaji wa sekta ya huduma, kupungua kwa uzalishaji wa zao la biashara la mwani na mapato ya leseni yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu. Wizara inaendelea kutekeleza jukumu lake la kuwawezesha wazalishaji katika Sekta ya kilimo kwa kuwapatia pembejeo, utaalamu na nyenzo za kufanyia kazi ili waongeze uzalishaji wenye tija.

## HALI YA UZALISHAJI

**8.** **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula, matunda na mboga umeongezeka kutoka tani 375,837.2 mwaka 2018 hadi kufikia tani 404,285 mwaka 2019, sawa na asilimia 7.6. Uzalishaji wa mazao ya chakula ikiwemo muhogo umeongezeka kutoka tani 156,077 mwaka 2018 hadi kufikia tani 177,299.02 mwaka 2019 sawa na asilimia 13.6, ndizi zimeongezeka kutoka tani 52,189 mwaka 2018 hadi kufikia tani 65,321.21 mwaka 2019 sawa na asilimia 25.2, viazi vitamu kutoka tani 52,582 mwaka 2018 hadi kufikia tani 53,996.25 mwaka 2019 sawa na asilimia 2.7; viazi vikuu kutoka tani 2,729.15 mwaka 2018 hadi kufikia tani 3,064.95 mwaka 2019 sawa na asilimia 12.3; mahindi kutoka tani 1,480.08 mwaka 2018 hadi kufikia tani 1,599.9 mwaka 2019 sawa na asilimia 8.1 na maboga kutoka tani 1,695.17 mwaka 2018 hadi kufikia tani 2,874.9 mwaka 2019 **(Kiambatanisho Nam. 1A).**

Kwa ujumla ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula hasa muhogo, ndizi, viazi vitamu, viazi vikuu, mahindi na maboga limetokana na hali nzuri ya hewa, kuongezeka kwa muamko wa wakulima katika kufuata miongozo na kanuni za kilimo bora, teknolojia na matumizi ya pembejeo bora za kilimo ikiwemo mbolea, dawa na mbegu bora wanayopatiwa kutoka kwa wataalamu wa sekta ya kilimo kupitia Wizara na Halmashauri za Wilaya.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mpunga umepungua kutoka tani 47,507.1 mwaka 2018 hadi tani 46,472 mwaka 2019 sawa na asilimia 2.2. Vilevile, uzalishaji wa mazao ya mboga na matunda umeshuka kwa asilimia 18 kutoka tani 52,667 mwaka 2018 hadi kufikia tani 43,080 mwaka

2019. Sababu zilizochangia kushuka kwa uzalishaji wa mazao haya ni mabadiliko ya tabia nchi yaliyopelekea mvua kubwa za vuli zilizonyesha hadi kufikia milimita 868 na kupelekea kuharibika kwa vipando na mazao hayo kwa wingi.

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mazao ya biashara ikiwemo karafuu na mwani, takwimu zinatuonesha uzalishaji wa zao la karafuu umeongezeka kufikia tani 1,691 kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na tani 675.2 za mwaka 2018. Hata hivyo, uzalishaji wa zao la mwani umepungua kwa asilimia saba (7) kutoka tani 10,424.9 mwaka 2018 hadi kufikia tani 9,663.2 mwaka 2019. Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa mazao hayo na kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora ya mikarafuu inayotolewa bila ya malipo pamoja na utowaji wa vifaa vya kilimo cha mwani ikiwemo taitai, kamba na vihori. Katika kuliendeleza zao la mwani WKMMU kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda zinaendelea na utafiti wa aina mpya ya mwani wenye tija wa aina ya Glacelaria, kuhamasisha kilimo cha mwani aina ya Cottonii kwa kuongeza uzalishaji na usarifu wa zao hilo.

11. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuongezeka kwa ekari zilizopandwa mazao ya kilimo mwaka 2019 hadi kufikia 97,576.3 kutoka ekari 95,021.2 zilizopandwa mwaka 2018, sawa na asilimia 2.7. Kati ya ekari hizo, ekari 10,000.9 sawa na asilimia 10.2 zilipandwa mazao ya mboga na matunda na ekari 87,575.4 zilizobakia zilipandwa mazao ya chakula sawa na asilimia 89.8.

12. **Mheshimiwa Spika,** kati ya ekari zote zilizopandwa mazao ya chakula, zao la muhogo ndilo lililochukua eneo kubwa

la upandaji wa ekari 30,204.3 sawa na asilimia 31. Zao la pili lilikuwa ni mpunga uliolimwa ekari 27,374.96 sawa na asilimia 28.05 zilizotumika kwa uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua na ekari 2,600.71 zilitumika kwa uzalishaji wa mpunga wa umwagiliaji maji. Viazi vitamu ni zao la tatu ambalo limepandwa ekari 7,713.75 sawa na asilimia 8.0. Aidha, eneo dogo la ekari 1,542.2 lilitumika kwa upandaji wa mazao ya jamii ya kunde, mtama, choroko na uwele. Wizara inatilia mkazo na kuhamasisha wakulima kulima mazao ya jamii ya kunde kwa vile ni chanzo kikuu cha protini itokanayo na mimea kwa kuwapatia mbegu bora za mazao ya kunde, choroko, mahindi na alizeti.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa mazao ya mifugo takwimu zinaonesha ongezeko la uchangiaji katika pato la taifa kutoka asilimia 6.1 kwa mwaka 2018 hadi kufikia 7.8 kwa mwaka 2019. Aidha, hali hiyo imetokana na ongezeko la mazao ya mifugo kwa uzalishaji wa tani 24,057 za nyama ya ng'ombe, nyama ya Mbuzi tani 2,317 na nyama ya Kuku tani 120,288. Vile vile, uzalishaji wa mayai umefikia 11,937,050 na maziwa lita 4,641,258. **(Kiambatanisho Nam. 1B, 1C na 1D)**

14. **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 35,441 mwaka 2018 hadi kufikia tani 36,728 mwaka 2019, ongezeko la asilimia 4. Mazao ya baharini yaliyosafirishwa nje ya nchi nayo yameongezeka kutoka tani 102.48 mwaka 2018 hadi kufikia tani 20,845.30 mwaka 2019 ikiwemo majongoo bahari, kaa na pweza **(Kiambatanisho Nam. 1E na 1F).** Aidha, Wizara kupitia Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) imeanza kazi za uvuaji wa samaki katika bahari kuu ambapo tunaamini kupitia boti

hizo idadi ya samaki watakaovuliwa itaongezeka maradufu na kuweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani na **la utalii.**

15. **Mheshimiwa Spika,** Misitu na rasilimali zinazotokana na msitu ikiwemo mbao, boriti na kuni zinamchango mkubwa katika maisha ya kila siku ya wananchi wa Zanzibar. Takwimu zinaonesha kwamba mwaka 2019 kiwango cha uzalishaji na matumizi ya kuni kwa mwaka 2019 umeongezeka kutoka mita za ujazo 26,569 mwaka 2018 hadi kufikia mita za ujazo 32,189 mwaka 2019, sawa na asilia 21.2. Vile vile, takwimu zinaonesha kushuka kwa uvunaji na matumizi ya boriti (majengo) kutoka 2,244.1 (2018) ikilinganishwa na uzalishaji wa mita za ujazo 1,721.1 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 23.3. Uzalishaji wa nguzo kubwa pia umepungua kwa mita za ujazo 3,115.1 mwaka 2019 sawa na asilimia 29.8. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kujengea nao pia umeshuka kutoka 3,182 mwaka 2018 hadi kufikia mita za ujazo 2,790 mwaka 2019 sawa na asilimia 12.3 ya ushukaji. Hali hii imetokana na juhudi inayochukuliwa na Serikali kwa kushirikana na jamii katika uhifadhi na kuleta maendeleo endelevu ya misitu. **(Kiambatisho Nam. 1G).**

16. **Mheshimiwa Spika,** takwimu za uchimbaji wa mchanga zinaonesha kupungua kwa asilimia 33 kutoka tani 948,329 mwaka 2018 hadi kufikia tani 639,602 mwaka 2019. **(Kiambatisho Nam. 1H)**. Uchimbaji wa mawe umepungua kutoka tani 132,434 mwaka 2018 hadi kufikia tani 103,513 mwaka 2019 sawa na asilimia 22. Vile vile, uvunjaji wa kokoto tani 52,440, kifusi tani 53,718 na chokaa tani 47.323 ikilinganishwa na uchimbaji wa mwaka 2019.

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

**17. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mipango Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (ATI). Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wakulima, wafugaji na wavuvi jambo ambalo limeongeza ari na hamasa na hatimae kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa eneo na kuwa na uhakika wa kuwepo kwa chakula nchini.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020

**18. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 10.46 bilioni** kutoka vianzio vyake 12 vya Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili, 2020 imekusanya jumla ya **TZS 5.73 bilioni** sawa na asilimia **55** ya makadirio. Kushuka kwa mapato kumechangiwa na kukosekana kwa mapato yatokanayo na leseni za uvuvi wa baharí kuu pamoja na kushuka kwa mapato ya maliasili zisizorejesheka **(Kiambatisho Nam. 2A na 2B)**

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 88.17 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 22.98 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za

kawaida (TZS 11.42 bilioni Mishahara na TZS 5.70 bilioni kwa Matumizi mengineyo na TZS 5.86 bilioni RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo). Jumla ya TZS 65.19 bilioni zimeidhinisha kwa kazi za maendeleo ikiwemo TZS. 60.26 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 4.93 bilioni kutoka SMZ.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili, 2020 Wizara imepatiwa jumla ya **TZS 44.51 bilioni,** kati ya hizo **TZS 17.27 bilioni** zilitumika kwa kazi za kawaida (TZS 8.55 bilioni mishahara; TZS 4.61 bilioni kazi za kawaida na TZS 4,11 bilioni Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Wakala wa Matrekta) na **TZS 27.23 bilioni** zilitumika kwa kazi za maendeleo (TZS 23.99 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 3.24 bilioni kutoka SMZ).
**(Kiambatisho Nam. 2C na 2D).**

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilitekeleza malengo yake kupitia Programu zake kuu tano ambazo ni:

a) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;

b) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka;

c) Programu ya Maendeleo ya Mifugo;

d) Programu ya Maendeleo ya Uvuvi; na

e) Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Wizara ilisimamia utekelezaji wa miradi na Programu 11 za maendeleo ikiwemo Program ya Miundombinu ya Masoko, uongezaji wa Thamani wa Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini - MIVARF, Mradi wa Usimamizi wa Kazi za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki ya Bahari ya Hindi - SWIOFish, Mradi wa Kuendeleza Zao la Mpunga - ERPP, Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima na Wazalishaji wa Mazao ya Mboga - Agri-Connect, Mradi wa Udhibiti wa Sumu Kuvu katika Mazao ya Nafaka - TANIPAC, Mradi wa Kukabiliana na Kilimo cha Mabadiliko ya Hali ya Hewa - Climate Smart Agriculture, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji, Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi, Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Sekta ya Kilimo, Mradi wa Usimamizi wa Matumizi ya Misitu ya Mwambao kwa Faida za Kiuchumi na Mradi wa Kutotolea Vifaranga vya Samaki.

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2019/2020

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imepata mafanikio yafuatayo:

a. Uzalishaji wa mpunga tani 46,472 katika eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na 13,000 Unguja);

b. Kuongezeka kwa wastani wa uzalishaji wa mazao ya matunda na mboga kutoka tani 42,989 kwa mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa tani 46,201 kwa mwaka 2019. Aidha, haya ni mapinduzi makubwa ya kilimo ambapo wakulima wameshajiika katika uzalishaji jambo ambali limeongeza kipato, ajira na kuimarika kwa lishe, afya ya jamii na Sekta Utalii;

c. Kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika hekta 47.5 katika mabonde ya Mtwango na Kwalempona. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa kutumia mabomba katika mabonde saba (7) yakiwemo Ole (ekari 9.2), Dobi (ekari 25), Machigini (ekari 28), Kibonde Mzungu (ekari 25), Koani (ekari 22), Mchangani (ekari 22) na Bandamaji (ekari 15) kupitia mradi wa ERPP umekamilika kwa asilimia 90. Vile vile, mafunzo ya kilimo Shadidi cha mpunga yametolewa kwa wakulima 1260 (750 Unguja na 510 Pemba);

d. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika hekta 500 umeanza kwa ujenzi wa mabwawa mawili (2) Kinyasini na Chaani. Kazi ya ujenzi inaendelea.

e. Malipo ya fidia TZS 663,606,850 (TZS 449,697,150 Unguja na TZS 213,909,700 Pemba) yamelipwa kwa wakulima 216 Unguja na Pemba katika mabonde ya Kinyasini, Mlemele na Makwararani. Aidha, Wakulima 191 walilipwa fidia za miti na mazao na wakulima 25 walilipwa fidia za nyumba na mali nyengine ili kupisha utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi

wa miundombinu ya Umwagiliaji maji. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inatarajia kufanya malipo ya fidia ya Tzs 1.3 bilioni hivi karibuni kwa wananchi katika maeneo ya chaani na Kinyasini;

f. Kukamilikia kwa tafiti 13 za kisayansi (3 kilimo, 5 mifugo na 5 uvuvi) pamoja na kuendelea na tafiti nyengine 27 (16 kilimo, 3 mifugo na 8 uvuvi). Aidha, Wizara imekamilisha matayarisho ya kongamano la utafiti la sekta ya kilimo kwa lengo la kutoa matokeo ya tafiti na mafunzo kwa watafiti; **(Kiambatanisho Nam. 3);**

g. Jumla ya miche 1,032,500 (849,960 ya misitu, 39,740 ya matunda, 106,000 ya minazi na 6,800 viungo na 30,000 mikarafuu) imeoteshwa katika vitalu vya Serikali sawa na asilimia 57.4 ya lengo. Wizara imepanda miti aina ya misitu, minazi, matunda, mikarafuu na viungo katika mashamba ya Serikali na maeneo yaliyochimbwa mchanga katika eneo la hekta 19.5 Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Nam. 4A);**

h. Tani 13.3 za asali zimezalishwa sawa na asilimia 88.6 ya lengo. Wafugaji wa nyuki 217 (wanawake 39 na wanaume 71) kwa Unguja na (wanawake 56 na wanaume 51) Pemba wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji wa asali. Aidha, katika kuhamasisha wafugaji hao mizinga 60 na vifaa vya ufugaji na urinaji wa asali vyenye thamani ya TZS 12,960,000 vimegawiwa;

i. Wizara imeimarisha huduma za kinga na tiba dhidi ya magonjwa ya wanyama kwa kuwapatia chanjo dhidi ya ugonjwa wa mahepe na Gumboro kuku 81,680 (Unguja 46,377, Pemba 35,303) na chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa 3,970 (Unguja 2,030, Pemba 1,940)

j. Kuimarisha huduma za upandishaji wa ng'ombe ambapo ng'ombe 1,010 aina ya Fresian na Jersey (Unguja 688 na Pemba 322) wamepandishwa kwa njia ya sindano sawa na asilimia 200 ya lengo **(Kiambatanisho Nam. 4B)**

k. Uzalishaji na ugawaji wa vifaranga vya samaki 195,000 umefanyika katika Shehia ya Bumbwini Makoba, Mafufuni, Jozani, Jadida, Kuu kuu na vifaranga vya majongoo 9,000 kwa Shehia ya Uzi, Uzi Ng'ambwa na Unguja Ukuu. Aidha, wafugaji 95 (wanawake 25 na wanaume 70) wa majongoo na samaki walipatiwa mafunzo ya uchimbaji wa mabwawa na ujengaji wa vizimba vya kufugia majongoo katika kijiji cha Uzi, Unguja Ukuu, Fundo na Pandani;

l. Kuimarisha uvuvi unaozingatia hifadhi ya mazingira kwa kuendeleza kamati 91 Unguja na Pemba ikiwemo:

- Kukamilika kwa ujenzi wa ofisi za hifadhi za TUMCA - Mkokotoni na Hifadhi ya CHABAMCA – Mazizini pamoja na kukamilika kwa kituo cha ulinzi wa bahari kilichopo katika kisiwa cha Pungume.

- Doria shirikishi 127 zilifanyika katika maeneo ya hifadhi ya bahari ikiwemo MINAI 56, MIMCA 41 na PECCA 30 ambapo mitego haramu 68 ilikamatwa.

- Utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi (Zanzibar Fisheries Master Plan)

- Ununuzi wa boti 3 za doria zilizowekwa katika hifadhi za TUMCA, CHABAMCA na Mkoa wa Kusini Pemba;

- Kukamilika kwa mipango mitatu ya uvuvi wa kipaumbele (samaki aina ya dagaa, pweza na samaki wa miambani)

m. Wafanyakazi 230 wamepatiwa mafao ya likizo yenye thamani ya TZS. 23,000,000, wafanyakazi 250 malipo ya muda wa ziada TZS. 18,010,815 na 34 wamepatiwa pesa za ubani TZS.10,200,000 baada ya kufiwa;

n. Ukusanyaji wa takwimu za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili umefanyika na ripoti imewasilishwa kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Aidha, utayarishaji wa Mpango Mkakati wa takwimu za Sekta ya kilimo umekamilika;

o. Sera na Sheria za Usimamizi na Uendelezaji wa Zao la Nazi zimekamilika. Vilevile, Wizara inaendelea na kampeni ya kitaifa ya uendelezaji wa zao la nazi nchini;

p. Rasimu ya Sera ya Kilimo, Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Zao la Nazi, Sheria ya Udhibiti na Uhifadhi wa Afya ya Mimea na Sheria ya Mbegu zimekamilika, hatua inayofuata ni kuidhinishwa katika vikao vya Uongozi Serikalini;

q. Wizara imekamilisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ZASDP) ya miaka 10 na kuanza utekelezaji. Programu hiyo imechangiwa jumla ya TZS. 20.2 bilioni sawa na Dola za Kimarekani 8.8 kutoka kwa Shirika la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kupitia Mradi mpya wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi. Aidha, fedha hizi zimeelekezwa katika kuimarisha uchumi wa buluu nchini. Vile vile Wizara imepata jumla ya TZS. 23 bilioni kutoka Jumuiya ya Ulaya kupitia Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima katika Kilimo cha Mboga na Matunda;

r. Kuendelea kutoa taaluma katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuwaunganisha wadau wa sekta na watoa huduma na masoko. Aidha, Wizara imefanikisha maonesho ya siku ya wakulima (Nanenane) yaliyofanyika Langoni/Kizimbani na ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Chamanangwe – Pemba;

s. Ununuzi wa Matrekta 20 kutoka Kampuni ya MAHINDRA kwa gharama ya TZS. 1.52 bilioni pamoja na Rotavator 7 zenye thamani ya TZS. 60 milioni umekamilika na tayari matrekta na zana hizo zimeshawasili Zanzibar;

t. Jumla ya ekari 20,138 (Pemba 13,609 na Unguja 6,529) zimechimbuliwa na kupandwa mpunga

u. Wizara imeanzisha utaratibu mpya wa ununuzi wa mbolea kwa ujumla kutoka China na imefanikiwa kupata mbolea kwa bei nafuu na kuwezesha kupata mbolea tani 100. Jumla ya tani 1,770 za mbolea (TSP tani 300, DAP tani 160 na UREA tani 1,310) zimenunuliwa. Vile vile, tani 279 za mbegu ya mpunga, na lita 21,000 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga **(Kiambatanisho Nam. 4C);**

v. Ukaguzi wa tani 103,469 za mazao yaliyoingia nchini ikiwemo mchele, unga wa ngano, mbatata, vitunguu, tungule, maharagwe, machungwa na tani 28,293 ya mazao yaliyosafirishwa nje ya nchi (karafuu, pumba za mahindi, ndimu, shokishoki, doriani) umefanyika; **(Kiambatanisho Nam. 4D);**

w. Jumla ya tani 338 za mchele zimenunuliwa kwa ajili ya hifadhi ya chakula cha akiba ambazo ziliuzwa kwa wananchi kwa kudhibiti mfumko wa bei ya mchele katika mwezi wa Ramadhani 2019. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na ZSTC inakamilisha ununuzi wa tani 220 za mchele kwa ajili ya chakula cha akiba;

x. Jumla ya watalii 61,372 (wa ndani 10,274 na wa nje 51,098) walitembelea Hifadhi za Jozani, Masingini, Kiwengwa Pongwe na Ngezi Vumawimbi. Aidha, Hifadhi ya Jozani na Ghuba ya Chwaka imepata tunzo

ya Tourism Award kwa kupokea watalii wengi kwa mwaka 2019;

y. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imetoa mgao wa TZS 226,399,589 kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2019 na TZS 413,941,996 kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2019 kwa jumuiya ya UWEMAJO, JECA na kamati 9 za vijiji vinavyoizunguka hifadhi ya Taifa ya Jozani kwa lengo la uhifadhi na kuendeleza miradi ya maendeleo kwa jamii;

z. Doria 246 zimefanyika (190 Unguja na 56 Pemba) Misumeno ya moto 77 imekamatwa na kuchomwa moto, magari 12 yaliosafirisha rasilimali za misitu bila kibali zilikamatwa pamoja na kesi 24 zilifikishwa Idarani kwa hatua za kisheria.

aa. Jumla ya tani 639,602 za mchanga na tani 137,671 za mawe, kifusi na kokoto zimechimbwa zenye thamani ya TZS 3,752,707,476 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo, wawekezaji pamoja na huduma kwa wananchi. Aidha, Wizara imelipa fidia ya vipando vyenye thamani ya TZS. 244,068,980 kwa wakulima 86 kwa ajili ya uchimbaji wa rasilimali za mchanga katika eneo la Fujoni na Kidanzini;

bb. Wafugaji 13,221 (6,770 wa ng'ombe, 1,899 wa kuku na 4,552 wa mbuzi/kondoo) walipatiwa elimu ya kinga na tiba za mifugo;

cc. Mitambo miwili (2) ya biogas imejengwa kwa upande wa Kiembe Samaki na Chuo cha Ufundi Karume Mbweni Unguja;

dd. Ununuzi wa mtambo wa kutengenezea chakula cha kuku na samaki wenye thamani ya TZS. 54,239,900 umenunuliwa wenye uwezo wa kuzalisha tani 50 kwa siku;

ee. Ujenzi wa jengo la Taasisi ya Utafiti na Maabara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini umeanza eneo la Maruhubi wenye thamani ya Dola za Kimarekani 700,000 kupitia mkopo wa Benki ya Dunia;

ff. Ununuzi wa boti tatu (3) mpya za doria zenye thamani ya Dola za Kimarekani 250,000 na ununuzi wa boti moja ya uvuvi (Sehewa 2) yenye thamani ya Dola za Kimarekani 508,000 (TZS 1.11 bilioni) kutoka Sri lanka umefanyika na boti zimewasili Zanzibar na kuanza kazi;

gg. Kuanza kwa ujenzi wa Soko la Samaki na Diko la Malindi. Aidha, Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameweka Jiwe la Msingi la ujenzi huo;

hh. Ununuzi wa vihori 250 kwa ajili ya wakulima wa mwani umekamilika. Aidha, Wizara inategemea kuvigawa kwa wakulima wa mwani Unguja na Pemba. Vifaa hivi vitawawezesha wakulima wa mwani kuweza kulima mwani wenye bei nzuri

na soko aina ya cottonii unaostawi katika kina kirefu cha maji;

ii. Tafiti 150 kuhusiana na uvuvi na mazao ya baharini zilizofanywa Zanzibar kuanzia mwaka 2000 zimekusanywa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi. Matokeo ya tafiti hizo yatafikishwa kwa wavuvi kwa kupitia semina, vipeperushi, majarida, radio na televisheni;

jj. Utafiti wa uchumi jamii kwa wavuvi wa kienyeji 450 umefanyika kwenye vijiji 20 Unguja na 10 Pemba, kwa lengo la kujua kipato na matumizi ya wavuvi ili kuweza kujua mbinu za kuwasaidia na kukuza kipato chao;

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**23. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Programu zake kuu tano (5) na ndogo kumi na tatu (13) ulikuwa kama ifuatavyo:

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

**24. Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo inajumuisha programu ndogo nne; Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji, Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo, Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

## Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji

**25. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Umwagiliaji Maji na ina jukumu la kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini kwa kutoa taaluma za uzalishaji na kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji maji.

## Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020

a) Kazi za ujenzi wa Mradi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji inaendelea kwa ujenzi kwa mabwawa, pamoja na ujenzi wa msingi mkubwa na midogo ya kupelekea maji shambani katika bonde la Kinyasini, Kibokwa na Chaani. Vile vile, matayarisho ya kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Kilombero, Cheju, Mlemele na Makwararani yameanza;

b) Utambuzi na uhakiki wa idadi ya wakulima wanaolima katika mabonde ya Kibokwa, Kinyasini na Chaani umekamilika. Kazi hiyo itaendelea katika bonde la Kilombero na Cheju kwa Unguja na Mlememe na Makwararani kwa Pemba;

c) Watalaamu 40 (25 Unguja na 15 Pemba) wa Wizara wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu za kitaalamu za usimamizi, ufatiliaji na ukaguzi wa kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji.

**26. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii iliombewa TZS 34.72 bilioni kati ya

hizo TZS 860.07 milioni kwa kazi za kawaida (TZS 560.07 milioni Mshahara, TZS 300.00 milioni kwa matumizi mengineyo) na TZS 33.86 bilioni kwa kazi za maendeleo (TZS 1.00 bilioni kutoka SMZ na TZS 32.86 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK). Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 programu imepata jumla ya TZS 6.08 bilioni sawa na asilimia 18 ya fedha zilizoombwa. Kati ya fedha hizo TZS 436.72 milioni kwa kazi za kawaida ikiwemo TZS 333.57 milioni mishahara na TZS 103.15 milioni kwa matumizi mengineyo. TZS 5.64 bilioni kwa kazi za maendeleo ikiwemo TZS 704.00 milioni kutoka SMZ na TZS 4.94 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK ya Korea.

***Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo***

27. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza Tafiti za Kilimo na Maliasili.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020**

28. **Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha wa 2019/2020, programu imetekeleza shabaha zifuatazo:

a) Jumla ya Tafiti nane (8) zimefanyika, kati ya hizo 5 zinazoendelea (2 mpunga, 1 pilipili boga, 1 matikiti maji, na 1 mangosteen) na 3 mpya zimeanza kufanyika ambazo ni utafiti wa mbegu za muhogo, mazao ya jamii ya kunde na kuangalia viwango vya mbolea (udongo);

b) Vikao viwili vya Baraza la Utafiti na viwili vya Kamati ya Wataalamu vimefanyika kwa ajili ya kupokea na kupitia Ripoti za Maendeleo za kazi za Taasisi;

c) Kazi ya ujenzi wa uzio wa mita 270 katika Shamba la Viungo na Utalii Kizimbani imeanza na ujenzi wa uzio wa mita 268 katika kituo cha Utafiti Matangatuani umekamilika. Aidha, ukarabati wa nyumba, ofisi na uimarishaji wa maeneo ya kuoteshea miche unaendelea katika kituo cha Kizimbani na Matangatuani;

d) Mafunzo juu ya utunzaji wa taarifa za utafiti (Research Data Management) yamefanyika Pemba kwa watafiti 10 (6 wanaume na 4 wanawake);

e) Sheria mpya ya Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Zanzibar imekamilika na kuanza kutumika;

f) Kuendeleza mashirikiano na Taasisi mbali mbali za kitaifa, kikanda na kimataifa zikiwemo ICIPE, IAEA, TAEC, IITA, AGRA, TOSCI, NAFAKA na IRRI katika tafiti za mazao ya mizizi na mpunga.

**29.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo iliombewa jumla ya **TZS 2.46 bilioni** (TZS 1.86 bilioni Mshahara na 600.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 Taasisi imepata **TZS 2.06 bilioni** (TZS 1.65 bilioni mishahara na TZS 414.60 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 84 ya fedha zilizoombwa.

## Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo

**30. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo inatekelezwa na Idara ya Kilimo na ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, utoaji wa pembejeo na kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalam kwa wakulima.

## Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020

**31. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha 2019/2020, program kupitia Idara imetekeleza yafuatayo:

a) Jumla ya ekari 20,138 (Pemba 13,609 na Unguja 6,529) zimechimbuliwa na kupandwa mpunga;

b) Tani 9 za mbegu za viazi lishe na tani 1 ya mbegu ya muhogo zimegawiwa kwa wakulima 257 wa Uzini, Mchangani, Bambi, Kitumba na Koani kwa Unguja na Mapofu, Tumbe, Kiuyu, Maziwang'ombe, Konde, Chimba, Mgogoni, Njuguni, Mtemani, Mjananza, Micheweni, Kinyasini, Pandani, Fundo, Kiungoni, Kambini, Mchangamdogo, Chwale, Kangagani, Kinyikani, Kiuyu, Mzambarauni, Ole, Uwandani, Vitongoji, Vikunguni, Mbuzini na Ziwani kwa Pemba. Aidha, wakulima waliopatiwa mbegu hizo walishauriwa kuwapatia wakulima wenzao;

c) Jumla ya Mitego 9,420 ya nzi waharibifu wa matunda imesambazwa kwa wakulima na mitego mengine 3,000 imeagizwa kupitia Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA). Aidha, Wizara kwa kushirikiana

na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) imeanza utekelezaji wa mradi wa kufanya tathmini ya kujua kiwango cha wadudu na uharibifu wa mazao ya matunda nchini;

d) Kuendelea na majaribio ya uzalishaji wa mazao ya viungo ikiwemo Vanilla, Pilipili Hoho, Manjano, Tangawizi na Pilipili Manga katika hekta tano za mashamba ya mipira Unguja na Pemba;

e) Jumla ya Miche ya minazi 106,000 (Unguja 60,000, na Pemba 46,000) imeoteshwa katika vitalu vya Serikali vinavyosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2019. Vile vile, Wizara imeendelea na ugawaji wa miche ya minazi 34,000 bila ya malipo katika msimu wa Vuli 2019.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu iliombewa **TZS 4.30 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.60 bilioni ni Mishahara na TZS 2.70 bilioni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata **TZS 3.81 bilioni** (TZS 1.21 bilioni mishahara na TZS 2.60 bilioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 88 ya fedha zilizoombwa.

## Programu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

33. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ambapo ina jukumu la kutoa huduma za matrekta kwa wakulima, sekta binafsi na taasisi; na kuhamasisha matumizi mazuri ya matrekta na zana za kilimo.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020**

a) Matrekta 47 yaliyopo Unguja na Pemba yamekaguliwa na kufanyiwa tathmini ya mahitaji ya vifaa. Matrekta 26, majembe 26 ya kuchimbulia na majembe 10 ya kuburugia yalifanyiwa matengenezo;

b) Jumla ya Matrekta 37 (Unguja 26 na Pemba 11) na majembe 10 ya kuburugia yalitoa huduma ya uchimbaji na uburugaji kwa mashamba ya wakulima;

c) Madereva na mafundi 40 (Unguja 25 na Pemba 15) walipatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo juu ya uendeshaji na utunzaji wa matrekta. Mafunzo hayo yaliyoendeshwa na wataalamu kutoka Kampuni za MAHINDRA & MAHINDRA na NEW HOLLAND.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **TZS 1.42 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 614.8 milioni ni mshahara na TZS 800.90 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 Wakala imepata **TZS 1.16 bilioni** (TZS 578.19 milioni mshahara na TZS 586.24 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 82 ya fedha zilizoombwa.

**Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe**

35. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa lengo la kuratibu upatikanaji wa chakula na lishe bora nchini, kufuatilia na kutathmini hali ya uhakika wa chakula na lishe kwa makundi mbali mbali ya wananchi na kitaifa.

### Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020

**36. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha 2019/2020, program kupitia Idara imetekeleza yafuatayo:

a) Jumla ya wanajamii 156 kutoka Shehia 35 za Wilaya ya Micheweni, Chake Chake na Wilaya ya Kaskazini ‘A’ walipatiwa mafunzo juu ya uhakika wa chakula na lishe. Aidha, wanakamati 40 kutoka Wilaya ya Kaskazini “A” walipatiwa mafunzo ya uhamasishaji ya lishe bora ya kilimo cha mboga na matunda. Shehia zilizofaidika na mafunzo hayo zimeaninishwa katika kiambatisho **(Kiambatisho Nam. 4E);**

b) Ukarabati wa Ghala la Akiba ya Chakula la Unguja liliopo Malindi umefanyika kwa kuimarisha mfumo wa hewa ikiwemo kuweka madirisha na taratibu za kuingiza mchele wa akiba zinaendelea. Aidha, Wizara inaendelea na matayarisho ya michoro kwa ajili ya ujenzi wa maghala mapya ya Hifadhi ya Chakula Pujini na Weni Pemba;

c) Wanajamii 1,267 walipimwa urefu na uzito wa mwili BMI (Body Mass Index) na kushauriwa utaratibu wa lishe kulingana na afya zao;

d) Jumla ya tathmini 3 za hali ya chakula na lishe nchini zimefanyika na kuwasilishwa kwa wadau. Aidha, muongozo wa matumizi ya chakula umeandaliwa kwa mashirikiano na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO);

e) Jumla ya wanajamii 24 kutoka Wilaya ya Kaskazini “A” na Kaskazini “B” walipata mafunzo ya juu ya

mfumo wa kukusanya taarifa ya hali ya chakula na lishe kwa kutumia teknolojia ya simu.

37. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **TZS 721.35 milioni** kwa kazi za kawaida (TZS 221.35 milioni Mshahara na TZS 500.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata **TZS 465.80 milioni** (TZS 192.54 milioni mishahara na **TZS 273.26 milioni** kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 65 ya fedha zilizoombwa.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka na ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, maliasili zisizorejesheka, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao sambamba na kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Program hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni Programu ya Maendeleo na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu na Programu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

### Programu Ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhifadhi misitu, wanyama pori pamoja na mazingira yao.

**Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2019/2020**

**40. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha 2019/2020, program imetekeleza yafuatayo:

a) Wafugaji wa nyuki 217 Unguja 110 (wanawake 39 na wanaume 71) na Pemba 107 (wanawake 56 na wanaume 51) wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji wa asali, usarifu wa bidhaa ya asali na kukabiliana na wadudu waharibifu. Aidha, mizinga 60 na vifaa vya ufugaji na urinaji wa asali vimegawiwa ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha wafugaji;

b) Mapitio ya mikataba mitatu (3) ya Usimamizi Shirikishi ya Misitu ya Jamii inayojumisha Shehia za Kibuteni, Charawe na Jendele yamefanyika kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya;

c) Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) inategemea kuongeza walinzi 30 kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usimamizi wa mradi wa Jozani na Ngezi;

d) Matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 1.4 kuelekea daraja la mikoko yamefanyika. Vile vile imeanza matayarisho ya ujenzi wa barabara ya kilomita 7.7 Wangwani yameanza;

e) Wizara imefanya mafunzo kwa watembezaji wageni kwa makampuni 15 yanaoleta wageni katika msitu wa Jozani

f) Wizara imefanya mapitio ya mchoro wa msitu wa jozani pamoja na kuweka majina ya miti na makobe kwa ajili ya kutoa taaluma na kuongoza watalii;

g) Andiko la kutangaza nia ya kuutangaza msitu wa Uzi – Vundwe (notice of intent) limetayarishwa. Aidha, Waraka wa pendekezo la kuweka muekezaji katika Msitu wa Uzi – Vundwe limetayarishwa kwa ajili ya kupelekwa Baraza la Mapinduzi kwa kupata mapendekezo;

h) Mazizi 15 yakiwemo JORIEFA, ZALA Park, UWEMAJO, Butterfly – Pete, Salim Zoo, Zanzibar Park, Hilal Zoo yametambuliwa na mazizi 8 yameanza hatua za usajili kwa kujaza fomu. Aidha, kanuni ya Zanzibar juu ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya wanyamapori, miti na mimea iliyohatarini kutoweka (CITES) na kanuni za usimamizi wa mazizi ya wanyamapori imezinduliwa na Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi;

**41.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu hii iliombewa jumla ya **TZS 342.8 milioni** kati ya hizo **TZS.114.6 milioni** kwa kazi za kawaida na **TZS 228.2** kwa kazi za Maendeleo. Hadi Machi, 2020 programu imepata **TZS 183.32 milioni** (**TZS 111.32 milioni** kwa matumizi ya kawaida na TZS 72.00 milioni kwa kazi za maendeleo) sawa na asilimia 53.5 ya fedha zilizoombwa.

**Programu Ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka**

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamia na kuratibu matumizi endelevu ya rasilimali zisizorejesheka

**Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2019/2020**

43. **Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha 2019/2020, program imetekeleza yafuatayo:

a) Hekta 2 zimerudishiwa kwa kupandwa miti katika maeneo yaliyochimbwa mchanga shimo la Donge Pangatupu kwa msimu wa vuli;

b) Rasimu ya Kanuni ya Maliasili Zisizorejesheka imekamilika na imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa hatua za mwisho;

c) Ripoti ya Utafiti juu ya namna bora ya urasimishaji na usimamizi katika uchimbaji wa kifusi, mawe na kokoto imekamilika na matokeo ya utafiti huo yamewasilishwa Serikalini;

d) Vikao 14 na ziara 2 za Kamati ya Uratibu na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka ya Baraza la Mapinduzi zimefanyika kwa ajili ya udhibiti na matumizi endelevu ya maliasili zisizorejesheka;

e) Matengenezo ya barabara inayokwendea katika chimbo la Fujoni lenye urefu wa kilomita mbili (2) uliogharimu TZS. 35,000,000 sambamba na uratibu

wa magari 680 yanayotoa huduma za upakizi na usafirishaji wa mchanga kutoka machimboni umefanyika;

f) Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeanzisha utaratibu mpya wa upatikanaji wa mchanga kwa wananchi pamoja na uvunaji na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali ya mawe, kifusi na kokoto;

**44. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **TZS 1.95 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. (TZS 1.67 bilioni ni mishahara na TZS 277.27 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata **TZS 2.15 bilioni** (**TZS 1.47** bilioni mishahara, **TZS 103.22** milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 579.40 kwa kazi za maendeleo) sawa na asilimia 110 ya fedha zilizoombwa.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**45. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utabibu wa Mifugo na Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo.

### Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo

**46. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uzalishaji wa Mifugo inalenga kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020**

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, program imetekeleza yafuatayo:

a) Ekari tisa (9) katika shamba la Kizimbani zimelimwa na kupandwa malisho ya mifugo aina ya Gugumua, Ukoka, Pemba Grass;

b) Mtambo wa kuzalisha gesi ya kuhifadhia mbegu za upandishaji ng'ombe kwa sindano umefanyiwa matengenezo;

c) Wizara imekamilisha tathmini ya utambuzi wa wafugaji na idadi ya mifugo iliyopo Unguja na Pemba kwa lengo la kupata takwimu sahihi za uzalishaji wa sekta ya mifugo. Tathmini imeonesha Zanzibar kuna jumla ya wafugaji 149,451, kati ya hao wafugaji wa ng'ombe wa kienyeji ni 53,864, ng'ombe wa maziwa (2,250), mbuzi wa kienyeji (23,439), mbuzi wa kisasa (1,182), kuku wa kienyeji (56,710), kuku wa mayai (1,906) na kuku wa nyama (9,800). Ongezeko la idadi ya wafugaji limepelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo ikiwemo maziwa, mayai na nyama. Hali hiyo, imeongeza upatikanaji na uhakika wa chakula na lishe;

d) Jumla ya watoa huduma za msingi vijijini (CAHW'S) 52 wamepewa mafunzo msasa ya matibabu ya mifugo na huduma za ugani Pemba;

e) Mikutano mitatu ya wafugaji wa ng’ombe wa maziwa (Cow shed) imefanyika Unguja kwa lengo la kuwaendeleza katika ufugaji wenye tija;

f) Vikundi sita vya ufugaji wa ng’ombe wa maziwa vilivyopo Machui, Mpapa na Fuoni Chunga vimeunganishwa na kiwanda cha maziwa cha Kampuni ya Azam kwa ajili ya kuuza maziwa yao. Aidha, lita 27,000 za lita za maziwa zinapelekwa kwa mwezi kutoka kwa wafugaji hao.

g) Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo ya Tanzania bara inaanzisha mashamba ya mfano ya uzalishaji wa ng’ombe chotara wa maziwa katika shamba la mifugo liliopo Pangeni.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo iliombewa jumla ya **TZS 303.56 milioni** (TZS 108.97 kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 194.60 milioni fedha za Mradi wa Miundombinu ya Mifugo kutoka SMZ). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata **TZS 41.33 milioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 14 ya fedha zilizoombwa.

## Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo

a) Sampuli 1,100 (Unguja 534 na Pemba 566) zimechunguzwa maradhi katika maabara ikiwemo ugonjwa wa kiwele, maradhi yanayoenezwa na kupe, ECF, babesiosis, anaplasmosis, heart water na chambavu, kuharisha damu na kuharisha chokaa;

b) Jumla ya wanyama 91,660 waliugua na kutibiwa magonjwa mbalimbali kati ya hao Ng'ombe 21,101, Mbuzi/Kondoo 5,575 Mbwa 1,724, Paka 956, Bata 156 Sungura 543 na Punda 60.

c) Ununuzi wa chanjo na reagents kwa ajili ya uchunguzi wa maradhi katika maabara za mifugo;

**49. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo iliombewa jumla ya **TZS 1.45 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.30 bilioni Mishahara na TZS 145.85 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata TZS 1.02 bilioni. (TZS 962.43 milioni Mishahara na TZS 59.72 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo) sawa na asilimia 70 ya fedha zilizoombwa.

**Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo**

**Utekelezaji wa Shabaha kwa mwaka 2019/2020**

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Tafiti 3 zimekamilika na tayari matokeo ya awali yameripotiwa zikiwemo Tathmini ya Ng'ombe wa Nyama Zanzibar, Tafiti za Aina ya Minyoo ya Ng'ombe na Tathmini ya Vyakula vya Kuku wa Nyama. Tafiti zimegundua kwamba ng'ombe wanaofugwa Zanzibar wana uzito mdogo wa nyama ukilinganisha na ng'ombe wanaotoka nje ya nchi. Vile vile, chakula cha kuku kilichotengenezwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kimethibitisha ubora wa virutubisho

na kupelekea ongezeko la nyama ukilinganisha na vyakula vyengine;

b) Wizara imetia saini mikataba miwili yenye thamani ya TZS milioni 570 kwa ajili ya ujenzi wa maabara na ofisi za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo huko Kizimbani na Chamanangwe.

c) Sheria ya Uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo imekamilika na kuanza kutumika;

d) Ujenzi wa mabanda ya utafiti wa kuku na mbuzi katika eneo la Taasisi lililopo Kizimbani umekamilika;

e) Mikutano miwili ya Bodi na Kamati ya Utafiti mmoja imefanyika kwa lengo la kuratibu na kuleta ufanisi wa utekelezaji wa malengo ya Taasisi;

**51.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, iliombewa jumla ya **TZS 2.06 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 305.70 milioni ni mshahara na TZS 556.50 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 1.20 bilioni fedha za Maendeleo kutoka SMZ). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata **TZS 689.17 milioni** (TZS 305.70 Mshahara na TZS 383.47 Matumizi ya kawaida) sawa na asilimia 34 ya fedha zilizoombwa.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza

uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii imegawika katika program ndogo mbili ambazo ni: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari; na Programu Ndogo ya Utafiti na Ufugaji wa Mazao ya Baharini.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari**

**53. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa bahari inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa mwaka 2019/2020**

**54. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Doria shirikishi 86 zilifanyika kwa kushirikiana na askari wa KMKM na kamati za uvuvi za shehia. Matokeo ya doria hizo mitego haramu 47 ilikamatwa na wahusika walifikishwa kituo cha polisi kwa mashtaka pamoja na leseni za uvuvi 1,296 na vyombo 403 zilikatishwa kutoka kwa wavuvi ambao hawakuwa na leseni na kuingiza mapato ya TZS 7,641,100/=;

b) Mkataba wa Ujenzi wa Chelezo kwa ajili ya boti za uvuvi za ZAFICO umeshasainiwa na tayari rasimu ya awali ya mchoro (engineering design) imeshawasilishwa Wizarani kwa maoni;

c) Mipango 3 ya usimamizi wa uvuvi wa vipaombele (samaki aina ya daga, pweza na samaki wa miambani) imeandaliwa;

d) Mpango wa ufungaji wa pweza kwa lengo la kuongeza kipato cha wavuvi umefanyika katika vijiji vya Uroa na Michamvi kwa Unguja na Pujini kwa Pemba.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ndogo hii iliombewa **TZS 19.4 bilioni** (TZS 763.78 milioni ni mishahara, TZS 200.00 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TZS 1.65 bilioni kutoka SMZ kwa miradi ya maendeleo na TZS 16.78 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata TZS 15.36 bilioni (TZS 559.58 mishahara, TZS 72.03 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 1.4 bilioni kutoka SMZ kwa miradi ya maendeleo na TZS 13.33 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo) sawa na asilimia 79 ya fedha zilizoombwa.

**Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini**

56. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mazao ya Baharini inalenga kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020**

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Taaluma ya mbinu bora za ufugaji ilitolewa kwa wafugaji 95 (wanawake 25 na wanaume 70) wa

majongoo bahari. Wafugaji wa samaki walipatiwa mafunzo ya uchimbaji wa mabwawa na ujengaji wa vizimba vya kufugia majongoo bahari katika kijiji cha Uzi, Unguja Ukuu, Fundo na Pandani. Mafunzo juu ya kuongeza thamani na ubora wa dagaa yametolewa kwa wajasiriamali 40 (36 wanaume na 4 wanawake);

b) Jumla ya wafanyakazi 11 wamepatiwa mafunzo ikiwemo (5 mafunzo ya uwezeshaji ufugaji wa jongoo bahari na ujenzi wa vishamba vya kufugia majongoo baharí; 4 ufugaji wa vifaranga vya samaki wa mwatiko na kaa nchini Philippine na wafanyakazi 2 walihudhuria mafunzo ya utotoleshaji wa vifaranga vya perege katika kituo cha kutotoleshea vifaranga kilichoko Bagamoyo;

c) Kituo kimeanza uzalishaji wa samaki aina ya *Marine tilapia na Milk fish* na wapo katika hatua ya viluilui. Vile vile, kituo kinaendelea kukuza samaki mama 40 wa aina ya mwatiko katika kituo cha uzalishaji vifaranga kiliopo Beit el Ras;

d) Jumla ya vikundi 23 vilisaidiwa vifaa vya kulimia mwani baada ya kupata mafunzo na kuanzisha shamba darasa, vifaa hivyo vikiwemo kamba roli 30, taitai roli 20 na vihori 30;

e) Ukaguzi wa usafirishaji wa mazao ya baharini ulifanyika kwa jumla ya tani 20,845.3 zenye thamani ya TZS 48.7 bilioni., ambapo jumla ya tani 9.663 za mwani zenye thamani ya TZS 5.6 bilioni zilisafirishwa;

f) Taaluma ya ukulima wa mwani katika kina kirefu

cha maji ilitolewa kwa vijiji 7 vinavyolima mwani ambavyo ni Pwani Mchangani, Pongwe, Muungoni na Bweleo kwa Unguja. Fundo, Makangale na Tumbe kwa upande wa Pemba. Pia vihori 10 kwa ajili ya kubebea mwani baada ya mavuno vilitolewa katika vijiji vya Kigunda, Kiwengwa, Uroa, Nyamanzi na Muungoni.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu hii ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini iliombewa **TZS 178.2 milioni** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata TZS 69.18 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 39 ya fedha zilizoombwa.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini**

**59.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini imetekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kukusanya taarifa za Utafiti kwa miaka 20 iliyopita (1999 - 2020) ambapo hadi sasa jumla ya ripoti za tafiti 700 zimepatikana;

b) Utafiti wa kipato na matumizi ya wavuvi wa kienyeji umefanyika kwa asilimia 50, ambapo taarifa za wavuvi zimeshakusanywa katika madiko 20 ya Unguja na madiko 11 ya Pemba;

c) Kukamilisha matayarisho ya utafiti wa mwani aina ya *Glacilaria* katika maeneo ya Nyamanzi na Muungoni ambayo yamechaguliwa kwa ajili ya utafiti huo;

d) Kuendeleza mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa kushiriki katika semina na mikutano;

e) Rasimu ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini imekamilika;

f) Ripoti ya kutambua maeneo bora ya kufuga majongoo bahari kwa Unguja na Pemba imekamilika.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini iliombewa jumla ya TZS 250 milioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata TZS 188.00 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 75 ya fedha zilizoombwa.

**Kampuni ya Uvuvi**

**61.** **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Kampuni ya Uvuvi ni kuanzisha Uvuvi wa kibiashara kwa kuimarisha ujenzi wa Miundombinu ya Uvuvi na kuelekeza nchi yetu katika uchumi wa Buluu.

**Utekelezaji wa Shabaha za Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO 2019/2020**

Kampuni imeweza kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Ununuzi wa Boti ya uvuvi (SEHEWA 02) umefanyika na boti hiyo imepokelewa Zanzibar tarehe 23/10/2019, na mafunzo kwa mabaharia yametolewa na hivi sasa imeanza kazi rasmi. Aidha, utaratibu wa ununuzi wa

Boti ya pili kutoka nchini Sri lanka umekamilika na ujenzi wa Boti hiyo unaendelea;

b) Matengenezo ya gari lenye jokofu lenye uwezo wa kusafirisha tani 10 za samaki kwa wakati mmoja umekamilika. Aidha gari hilo lenye thamani ya TZS 299,892,401 linatarajiwa kufika nchini mwishoni mwa mwezi wa Aprili,2020;

c) Jumla ya tani 3.5 za samaki aina ya Nduwaro, Mbasi, Sehewa na Jodari zimevuliwa kwa majaribio kutoka bahari kuu na kuuzwa kwa thamani ya TZS. 20,000,000;

d) Ufungaji wa mtambo wa kuzalishia barafu katika Soko la Malindi-Bandarini umekamilika;

e) Ujenzi wa eneo la Mitambo ya baridi pamoja na kiwanda cha usarifu wa minofu ya samaki Malindi Zanzibar upo katika hatua ya michoro ambapo Kampuni iliyokabidhiwa kazi hiyo tayari imewasilisha michoro kwa mara ya tatu kwa ZAFICO ili kufanyia mapitio na masawazisho;

f) Utafiti bainishi (Feasibility study) katika mnyororo mzima wa biashara ya madagaa Zanzibar umekamilika na umebaini kuwa, ZAFICO inaweza kuwekeza katika biashara ya dagaa na kupata faida bila ya kufanya ushindani na wafanya biashara wadogo waliojiwekeza katika sekta hiyo hapa nchini;

g) Mkataba wa Makubaliano ya msingi (MoU) Baina ya ZAFICO, Willing hand ya nchini Norway na

Onyxstone ya Oman kwa ajili ya uanzishwaji wa shamba la ufugaji wa samaki baharini (Cage Fish farm) umesainiwa mwezi wa Novemba, 2019;

h) Wafanyakazi 15 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi wakiwemo; Msimamizi wa misafara ya meli mmoja (1), Manahodha wawili (2), Wahandisi wawili (2) na Mabaharia wa kawaida 10 tayari wamepatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo juu ya dhana nzima ya uvuvi wa kaputi kwa kutumia meli ya uvuvi, namna ya kutengeneza mtego wa kaputi, na kuvua kwa kutumia mtego wa kaputi kwa meli ya uvuvi.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Kampuni ya Uvuvi ZAFICO ilitarajia kupata jumla ya **TZS 9.8 bilioni** ikiwa ni pato litokanalo na mchango wa wana Hisa wake (ZSSF, ZSTC, ZIC na ZPC) pamoja na pato litakalotokana na uzalishaji wake kwa kipindi hicho. Aidha, inatarajiwa kutumia jumla ya TZS 9.6 bilioni (TZS 3.2 bilioni kwakazi za kawaidana TZS 6.4 bilioni kwa ajili ya uwekezaji). Hadi kufikia Machi, 2020 Kampuni imetumia TZS 1.31 bilioni kwa kazi za kampuni sawa na asilimia 19 ya fedha zilizoombwa.

## PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA

**63.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inayojumuisha programu ndogo tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara, Programu ndogo ya Uendeshaji na Utawala na Programu Ndogo ya Utawala na Ofisi Kuu Pemba.

### Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara

**Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti, pamoja na kuratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

### Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020

**64.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Nakala 500 za Kitabu cha Mwenendo wa takwimu za Sekta ya kilimo na nakala 500 za Jarida la Mkulima zimechapishwa na kusambazwa kwa wakulima;

b) Utafiti wa Mkaa poa pamoja na matayarisho ya utafiti wa tathmini za maliasili za mawe na kokoto unaendelea;

c) Vikao 2 vya maandalizi vya mkutano mkuu wa Baraza la utafiti vimefanyika, ambapo tafiti 46 zimepitishwa kwa ajili ya mkutano wa Baraza la utafiti;

d) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo imekamilika na kujadiliwa katika Kamati ya Mawaziri wa Sekta ya Kilimo inayoongozwa na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar; Aidha, programu imeshaanza kuchangiwa jumla ya TZS. 23.3 bilioni kutoka

Jumuiya ya Ulaya kwa utekelezaji wa Mradi wa Agri-conect, TZS. 20.2 kutoka Shirika la kimataifa la IFAD kwa ajili ya kutekeleza Mradi ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi na TZS 11.5 bilioni kutoka Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani GEF;

e) Ziara ya kutathmini utekelezaji wa Miradi na Programu zilifanyika kwa Miradi wa Kilimo Himilivu (Climate Smart Agriculture);

f) Mikutano mitano (5) ya mashirikiano kati ya SMT na SMZ imefanyika kwa sekta za Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, na Wizara ya Ardhi imefanyika Dodoma. Aidha, mikutano miwili ya washirika wa maendeleo (DPs) imefanyika. Mkutano mmoja wa washirika kutoka Cuba pia umefanyika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ya Mipango na Utawala iliombewa jumla ya **TZS 17.73 bilioni** (TZS 5.29 bilioni ni mshahara, TZS 1.17 kazi za kawaida, TZS 885.40 milioni ni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ na TZS 10.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata jumla ya **TZS 6.62 bilioni** (TZS 214.81milioni mishahara; TZS 200.99 milioni kazi za kawaida; (**TZS 5.65 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 554.00 milioni kutoka SMZ) sawa na asilimia 37 ya fedha zilizoombwa.

## Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inatekeleza na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Madhumuni ya programu hii ni kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, programu inaratibu masuala mtambuka ikiwemo Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

## Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020

**66.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Wafanyakazi 47 wamejengewa uwezo wa kitaaluma (3 PhD, 4 MSc, 26 BSc, 10 Diploma, 3 Cheti na 1 Short course);

b) Mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa wafanyakazi 24 ikiwemo nchini Korea, India, Japani, kenya na Indonesia katika fani za kilimo, uvuvi na ufuatiliaji na thathmini

c) Wizara imeajiri wafanyakazi wapya 339 ikiwemo madaktari watano wa wanyama, wahudumu wa mashambani 97 wanaotoka katika maeneo husika na fani mbali mbali za sekta ya kilimo. Vile vile, Wizara imeorodhesha majina ya wataalam 317 wa ngazi ya Shahada ya kwanza, Shahada ya uzamili na Shahada

ya Uzamivu kwa ajili ya kuongeza wataalamu katika taasisi za utafiti na maidara;

d) Wizara imekamilisha utafiti wa uzalishaji wa utomvu katika mashamba ya mipira yenye hekta 1,270 (Unguja hekta 637 na Pemba hekta 633). Aidha, takwimu zinaonesha kwamba uzalishaji wa utomvu katika mashamba hayo umepungua na Wizara imekamilisha mpango wa uendelezaji wa mashamba hayo kwa matumizi mengineyo yenye tija na kuongeza pato la taifa;

e) Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi imekamilisha upimaji wa mashamba ya mikarafuu 70 yaliyopo Wilaya ya Micheweni na inaendelea na upimaji wa mashamba katika Wilaya ya Wete kati ya mashamba 732 yaloidhinisha kutolewa kwa wananchi;

f) Wizara imesimamia ukodishaji wa mashamba ya eka 875 na mashamba matano makubwa yanayosimamiwa na WKMMU yaliyopo kisiwani Pemba na kukodisha mashamba matatu yaliyopo Kizimbani. Jumla ya TZS 716,084,000 zimekusanywa kutoka katika mashamba hayo. Aidha, Wizara imelipa kifuta jasho cha TZS. 60,296,000 kwa ajili ya wananchi wanaosimamia mashamba hayo;

g) Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo na ZAWA imeweza kufanya usafi na uungaji wa huduma ya maji katika shamba la Makuwe. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na ZECO iko katika hatua za mwisho za kufanya tathmini za mwisho katika hatua za upelekaji umeme katika shamba hilo;

h) Wizara imekamilisha matengenezo ya kituo cha mifugo kilichopo Ole pamoja na ujenzi wa uzio katika kituo cha karantini kilichopo Gando-nzi wengi pamoja na uwekaji wa miundombinu ya maji katika shamba la mbegu Bambi.

i) Kitengo cha Wakaguzi wa ndani kimehakiki mapato na matumizi ya Serikali katika Idara na Taasisi zilizochini ya Wizara. Aidha, Kitengo cha Manunuzi cha Wizara kimefanya vikao 30 vya zabuni na tathmini ya manunuzi ya vifaa na huduma kwa kampuni kupitia Miradi na Taasisi zake;

j) Watarajiwa wastaafu 20 wamepatiwa mafunzo ya kustaafu kazi.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ndogo ya utawala na mafunzo, iliombewa jumla ya **TZS 2.34 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.84 bilioni ni mishahara na TZS 500.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepatiwa **TZS 1.88 bilioni** (TZS 1.19 bilioni kwa mishahara na TZS 690.41 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 80 ya fedha zilizoombwa.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara**

**Pemba Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2019/2020**

**68.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuratibu na kufanikisha vikao vinne na ziara za Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;
b) Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;

c) Vikao 24 vya uendeshaji na usimamizi wa ofisi kuu pemba vimefanyika kwa kushirikiana idara na taasisi mbali mbali mtambuka za sekta ya kilimo-Pemba;

d) Uratibu wa ziara za wageni na viongozi wa Wizara umefanyika kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Wizara pamoja na kuhudhuria katika sherehe na kumbu kumbu za kitaifa Pemba;

e) Mashirikiano na taasisi nyenginezo (Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii) yameimarishwa.

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, iliombewa **TZS 3.55 bilioni** (TZS 3.20 bilioni mishahara na TZS 350.00 milioni ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2020 programu imepata **TZS 2.69 bilioni** (TZS 2.41 bilioni mishahara na TZS 284.18 milioni kazi za kawaida) sawa na asilimia 76 ya fedha zilizoombwa.

## CHANGAMOTO

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada za Wizara na Serikali kwa ujumla, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na:

a) Uvamizi wa ardhi za kilimo na misitu kutokana na kuongezeka kwa makaazi na miradi mengine ya maendeleo;
b) Kuongezeka kwa bei ya pembejeo za Kilimo;
c) Wakulima kuchelewa na kutokuchangia katika kupatiwa huduma za matrekta.
d) Mahitaji makubwa ya rasilimali ya mchanga kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo na wawekezaji nchini.
e) Wizi na uchimbaji holela wa rasilimali ya mchanga
f) Ongezeko la mvua za vuli zaidi ya wastani zilizopelekea kushuka kwa uzalishaji wa mpunga pamoja na mazao ya mboga na matunda.
g) Kujitokeza kwa migogoro na uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi.
h) Kuzuka kwa maradhi ya Homa Kali ya Mapafu (Korona) inayosababishwa na virusi ya COVID-19, kunahatarisha hali ya usalama wa chakula nchini hasa kuwepo kwa uwezekano wa kupungua kwa uingizaji wa chakula kutoka nje ya nchi. Aidha, uvuvi katika ukanda wa Bahari Kuu pia unatarajiwa kupungua na hivyo kupelekea kushuka kwa mapato ya Serikali.

   Kabla ya kuzuka kwa maradhi ya Korona, Mamlaka ya Bahari kuu ilikuwa imeingia mikataba ya uvuvi na makampuni 51, lakini utekelezaji wa mikataba hiyo kwa sasa umesimama.

## HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

a. **Uvamizi wa ardhi za kilimo na misitu kutokana na kuongezeka kwa makaazi na miradi mengine ya maendeleo;**
Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi kuyatambua, kuyapima na kuyapatia Hati Miliki maeneo ya Kilimo.

b. **Kuongezeka kwa bei ya pembejeo za Kilimo;**
Wizara imeweka utaratibu mzuri wa ununuzi wa pembejeo kwa njia ya ujumla (bulk purchase) kutoka viwandani nchini China ambapo pembejeo hiyo imepatikana kwa bei nafuu mara dufu ikilinganishwa na makapuni yaliopo Tanzania.

c. **Mahitaji makubwa ya rasilimali ya mchanga kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo na wawekezaji nchini.**
Wizara imeweka utaratibu mzuri wa utoaji wa huduma ya mchanga kwa miradi mikubwa ya maendeleo, wawekezaji na wananchi

d. **Wakulima kuchelewa na kutokuchangia katika kupatiwa huduma za matrekta.**
Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeandaa utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa fedha za mchango kwa ajili ya huduma za matreka ambapo jumla ya **TZS 43,112,000** zilikusanywa kwa msimu wa masika 2020.

e. **Wizi na uchimbaji holela wa rasilimali ya mchanga**
Wizara kwa kushirikiana na vikosi vya SMZ imeunda kikosi shirikishi cha doria ambacho kinaendelea na kupambana na wizi na uchimbaji wa mchanga kiholela pamoja na udhibiti wa ukataji ovyo wa miti.

f. **Ongezeko la mvua za vuli zaidi ya wastani zilizopelekea kushuka kwa uzalishaji wa mpunga pamoja na mazao ya mboga na matunda.**
Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imechukua hatua mbali mbali za kukabiliana na hali iliyojitokeza kwa ununuzi wa Rotavator saba (7) kwa ajili ya matayarisho ya kilimo cha mpunga katika maeneo yanayotuama maji pamoja na ununuzi wa tani 29 za mbegu ya mpunga wa muda mfupi, alizeti, mahindi, chooko, kunde na mbegu za viazi vitamu zimenunuliwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji ili kuepuka changamoto ya upungufu wa chakula nchini. Aidha, Wizara inaendelea na kuhamasisha wananchi kulima mazao ya mboga na matunda kwa matumizi ya mashamba vizimba (greenhouse) kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

g. **Kujitokeza kwa migogoro na uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi.**
Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri husika na KMKM inaimarisha doria shirikishi katika maeneo ya hifadhi. Vile vile, wizara imeongeza vituo vya hifadhi ikiwemo TUMCA na CHABAMCA pamoja na kituo cha doria katika kisiwa cha Pungume na ununuzi wa boti tatu za doria.

h. **Kuzuka kwa maradhi ya Homa Kali ya Mapafu (Korona) inayosababishwa na virusi ya COVID-19.** Wizara imechukuwa hatua mbali mbali katika kukabiliana na athari za maradhi ya Korona katika Sekta ya Kilimo na hatua zilizochukuliwa ni pamoja na;

- Wizara imetayarisha Mkakati wa kukabiliana na athari za maradhi ya Korona kwa kipindi cha sasa na miaka miwili baada ya kumalizika kwa maradhi haya. Mkakati huo umejikita katika kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na huduma za uzalishaji;

- Wizara imenunua zana za utayarishaji wa ardhi (Rotavator) saba ili kuongeza kazi ya utayarishaji wa maeneo ya mpunga yaliyoingia maji na kuongeza uzalishaji wa mpunga;

- Wizara kwa kushirikiana na Shirika la ZSTC la Wizara ya Biashara na Viwanda inakamilisha utaratibu wa kununua mchele kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula;

- Wizara imefanya vikao na halmashauri kuweka mikakati ya kuhamasisha wakulima, wavuvi na wafugaji kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, mifugo na uvuvi. Wizara hivi sasa inakalimilisha utaratibu wa kununua mbegu tani 20 za mazao ya mahindi, alizeti, choko na tani 300 za mbegu za viazi vitamu. Mbegu hizi zitatolewa kwa wakulima bure.

- Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi Wizara imeshirikiana na Halimashauri za Wilaya na Kamati za Uvuvi katika kutowa mafunzo na miongozo kwa Vijana ambao waliojiingiza katika Uvuvi baada ya kusimama shughuli za Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto hizi zilizokuwepo ambazo tumeanza kuchukuwa tahadhari kujikinga na upungufu wa chakula, hali ya chakula Nchini iko vizuri na upatikanaji wa bidhaa za chakula kwaajili ya mwezi wa Ramadhani ni wakuridhisha.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

## MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKAWA FEDHA 2020/2021

**71.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 10.47 bilioni** kutoka vianzio vyake 12 vya Unguja na Pemba **(Kiambatanisho nam. 5A)**.

## MAKADIRIO YA MATUMIZI 2020/2021

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu tano ambazo ni:

a) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;

b) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka;

c) Programu ya Maendeleo ya Mifugo;

d) Programu ya Maendeleo ya Uvuvi; na

e) Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Wizara itaendelea na utekelezaji wa Miradi na Programu kumi (10) ya Maendeleo ikiwemo SWIOFish, Mradi wa Uendelezaji wa Zao la Mpunga – ERPP, Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi-Zanzibar, Mradi wa Kuendeleza Uzalishaji wa Mazao ya baharini, Agri-Connect, TANIPAC, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji, Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Sekta ya Kilimo, Mradi wa Kuangamiza Wadudu Waharibifu wa Matunda, Mradi wa Usimamizi wa Matumizi wa Misitu ya Mwambao na, Ujenzi wa Soko la Malindi **(Kiambatisho Nam. 6A-6G)**

**73.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kutekeleza programu hizo kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 Wizara inaombewa kutumia jumla ya **TZS 129.86 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 23.32 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS 11.47** bilioni Mishahara na TZS 5.22 bilioni matumizi mengineyo na TZS **6.63** bilioni RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao Baharini, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo **(Kiambatisho Nam. 5B).** Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa

**TZS 106.54 bilioni** (**TZS 83.54 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 23.00 bilioni kutoka SMZ, **(Kiambatisho Nam. 5C)**.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na uvuvi inathamini mchango wa Serikali pamoja na kutoa kipaombele cha pekee katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini. Aidha, kumekuwa na ongezeko la fedha za bajeti ya utekelezaji wa malengo ya Wizara kutoka TZS. 88.17 bilioni kwa mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na bajeti ya TZS. 129.86 kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 47.3.

**MALENGO YA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**75.** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuendeleza kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imejiwekea malengo yafuatayo kupitia programu zake tano:

a. Kupima, kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji maji hekta 600 katika mabonde ya Chaani, Kilombero na Cheju pamoja na ujenzi wa mabwawa 2, visima 16 na mitaro ya umwagiliaji kupitia mradi wa EXIM BANK wa Korea.

b. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika eneo la hekta 65 na kukarabati hekta 87 kupitia mradi wa ERPP pamoja na kukarabati hekta 87.

c. Kuongeza uzalishaji wa Mpunga kufikia wastani wa tani 50,000 pamoja na kuendelea kutoa huduma za

matrekta na zana zake kwa wakulima na kufuatilia ukulima wa zao la mpunga katika eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na Unguja 13,000) pamoja na mazao mengine ya kilimo;

d. Kuotesha miche 3,000,000 (500,000 Mikarafuu, 500,000 Minazi, Misitu 1,500,000 na 500,000 ya matunda na viungo) katika vitalu vya Serikali.

e. Kufanya tathmini ya kujua kiwango cha wadudu pamoja na athari ya uharibifu wa matunda unaosababishwa na nzi wa matunda;

f. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Usimamizi wa Misitu, Sera na Sheria ya Uvuvi, Sheria ya mbegu na Sheria ya Utibabu na udhibiti wa mimea na Sheria ya Kuanzishwa kwa Taasisi ya Uvuvi na Mazao Baharini pamoja na kutayarisha Mpango Mkakati wa Sera ya Kilimo, Maendeleo ya Mifugo pamoja na kukamilisha Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini;

g. Kutayarisha Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ZASDP;

h. Kufanya tafiti 26 za kisayansi (16 kilimo, 5 mifugo na 5 Uvuvi), tafiti za kiuchumi na Kijamii kwa mujibu wa Zanzibar Research Agenda, kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi na kuimarisha miundombinu ya utafiti;

i. Kuongeza uzalishaji wa asali kutoka tani 13.3 hadi 25 kwa kuwawezesha wazalishaji wakubwa 15 wa nyuki (Pemba 10 na Unguja 5) kuzalisha kibiashara pamoja na kuanzisha mabanda darasa 13 ya ufugaji wa nyuki.

j. Kuongeza uzalishaji na kufanya utafiti wa kujua idadi ya wanyama adimu na mazingira yao wakiwemo Paa Nunga, Popo na Paa Chesi wa Pemba.

k. Kudhibiti uchimbaji na usafirishaji haramu wa maliasili zisizorejesheka kwa kufanya doria 100 katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

l. Kurejeshea maeneo yaliyochimbwa mchanga hekta 40 pamoja na kubuni miradi mbalimbali itayoweza kufanyika katika maeneo hayo kwa kushirikiana na wanavijiji katika maeneo ya Pangatupu na Donge chechele.

m. Ununuzi wa mchele tani 338 za hifadhi ya chakula cha akiba pamoja na kuanza kwa ujenzi wa maghala matatu ya uhifadhi wa chakula;

n. Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi kuyatambua, kuyapima na kuyapatia Hati Miliki maeneo ya Kilimo;

o. Kukamilisha ujenzi wa maabara na ofisi ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini pamoja na ujenzi wa kituo cha kuimarisha ulinzi Jambiani na bwawa la kupokea vifaranga vya samaki kisiwani Pemba;

p. Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira kwa kamati 91 za uvuvi Unguja na Pemba na kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini kibiashara na kuendelea kutoa mafunzo kwa kamati za mwani 83 Unguja na Pemba;

q. Ununuzi wa boti tano (5) ya uvuvi ya Kampuni ya ZAFICO pamoja na kuanzisha mashamba manne (4) ya Majongoo kibiashara;

r. Kuongeza uzalishaji wa kuku wa nyama hadi kufikia tani 4,969.64, mayai treya 4,946,695.4 na maziwa hadi kufikia lita 6,046,732.8;

s. Kuzalisha chakula cha kuku na samaki tani 14,000 kwa mwaka kwa kutumia formula mpya;

t. Kupandisha ng'ombe 2,500 (Unguja 1,500 na Pemba 1,000) kwa sindano;

u. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 1,200 ikiwemo malipo ya likizo, muda wa ziada na pesa za ubani kwa wafiwa pamoja na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;

v. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 51 (1 PhD, 1 MSc, 48 Digirii na Diploma 1) wanaoendelea na masomo.

## SHABAHA ZA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021
## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

**76. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Kilimo Pragramu hii imegawika katika programu ndogo nne ambazo ni:

a) Programu ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji;

b) Programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo;

c) Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo;

d) Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo;

e) Programu ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa jumla ya **TZS 79.03 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 5.57** ambapo (**TZS 3.17 bilioni** matumizi kawaida na **TZS 2.39 bilioni** ni Mishahara). Wizara pia inatarajia kupata Ruzuku ya TZS **5.21 bilioni** ambapo **TZS 2.03 bilioni** matumizi kawaida na TZS **3.17 bilioni** ni Ruzuku ya Mishahara kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Vilevile, Programu inaombewa jumla ya **TZS 68.24 bilioni** kwa miradi ya maendeleo (TZS 48.24 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 20.00 bilioni kutoka SMZ).

## Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji kwa Mwaka 2020/2021

**78.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji wa hekta 600 katika mabonde ya Chaani, Kilombero na Cheju pamoja na ujenzi wa

mabwawa ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Makwararani na Mlemele;

b) Ulipaji wa fidia ya mazao kwa wakulima watakaoathirika wakati wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Chaani, Kinyasini, Cheju, Makwararani na Mlemele.

c) Utambuzi na uhakiki wa idadi ya wakulima katika mabonde yatakayoendelezwa miundombinu ya umwagiliaji yakiwemo Kilombero, Cheju, Makwararani na Mlemele.

d) Kuimarisha jumuiya za wakulima wa umwagiliaji maji kwa kushirikiana na Halmashauri;

e) Kusimamia na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji maji kwa kushirikiana na Halmashauri husika;

f) Kuhamasisha na kutoa elimu juu ya matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji maji ikiwemo ujenzi wa mashamba ya vizimba na kilimo cha kutumia paipu;

g) Kulipa fidia, uungaji wa umeme katika skimu mpya na ugawaji wa ploti 6,000 za umwagiliaji maji.

h) Kufanya uhakiki na kuorodhesha majina ya wakulima wanaolima katika maeneo ya Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji maji.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 67.96 bilioni** ambapo (TZS 563.91 milioni Mshahara, TZS 312.57 milioni kwa matumizi mengineyo na **TZS 67.09 bilioni** fedha za maendeleo (TZS 19.90 bilioni kutoka SMZ na TZS 47.19 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo
EXIM BANK).

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo kwa mwaka 2020/2021**

80. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu Ndogo hii ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo inalenga kutekeleza yafuatayo:

a) Kufanya tafiti 16 za mazao ya kipaombele (tafiti 14 zinazoendelea na tafiti 2 mpya (1 ya sayansi ya chakula na 1 ya maliasili).

b) Kuimarisha miundombinu ya Utafiti wa kilimo ikiwemo Maabara, Mashamba vizimba (green house na screen house) pamoja na Vituo vya Utafiti vya Wesha, Tumbe, Bambi, Makunduchi, Kijichi na Selem.

c) Kuimarisha ujenzi na usimamizi wa Shamba la Viungo la Kizimbani kwa kujenga uzio, vyoo na sehemu ya mapokezi kwa wageni na watalii.

d) Kuimarisha rasilimali watu kwa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 35 na kugharamia mafunzo ya shahada ya juu kwa wafanyakazi 4.

e) Kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi za utafiti na ununuzi wa vifaa na huduma kwa ajili ya ofisi ikiwemo ununuzi wa gari moja (pickup) na pikipiki 3 pamoja na kukarabati ofisi na nyumba za wafanyakazi.

f) Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (2014 – 2019).

g) Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za Utafiti za Ndani, Kikanda na Kimataifa.

**81. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inaombewa jumla ya TZS 3.05 bilioni (TZS 2.39 bilioni Mshahara na 660.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Kilimo Mwaka 2020/2021**

a) Kununua na kusambaza tani 207 za mbegu ya mpunga, tani 500 za mbolea (TSP tani 300 na DAP tani 200) na lita 21,000 za dawa ya kuulia magugu.

b) Kutoa elimu ya uzalishaji katika zao la mpunga kupitia mabonde 10 ya mfano (6 Unguja - Kilombero, Mchangani, Muyuni, Tomondo, Mkanyageni na Kibonongwa na 4 Pemba - Mfubaha, Maotwe, Ngwia na Mavuika);

c) Kufuatilia uzalishaji wa mpunga eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na 13,000 Unguja);

d) Kusambaza mbegu ya muhogo na viazi lishe kwa wakulima 500;

e) Kutoa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo karafuu pamoja na kusimamia udhibiti wa nzi waharibifu wa matunda.

f) Kuotesha Miche 1,200,000 (500,000 Mikarafuu, 500,000 Minazi na 200,000 ya matunda na viungo) katika vitalu vya Serekali.

g) Kuendelea na kufuatilia uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi ikiwemo Vanilla, Pilipili Hoho, Manjano, Tangawizi na Pilipili Manga katika eneo la hekta 10 za mashamba ya mipira Unguja na Pemba.

h) Kutoa elimu juu ya matumizi bora ya pembejeo za kilimo kupitia mashamba darasa kwa kushirikiana na Halmashauri;

i) Kuhamasisha wakulima matumizi ya mbinu bora ya kilimo hai kwa kushirikiana na Halmashauri;

j) Kuhamasisha uzalishaji wa zao la korosho na alizeti kwa kushirikiana na Halmashauri;

**82.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu inaombewa. **TZS 4.23 bilioni** kati ya hizo TZS. 4.01 ni kwa matumizi ya kawaida (TZS 1.61 bilioni ni Mishahara na TZS 2.40 bilioni kwa kazi za kawaida), kwa fedha za Maendeleo Programu inaombewa jumla ya TZS. 220 (TZS 100 milioni kutoka SMZ na TZS 120 milioni kutoka kwa washirika wa maendeleo).

**Shabaha Zitakazotolewa na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa Mwaka 2020/2021**

a) Kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima, sekta binafsi na taasisi nyengine;

b) Kuchimba na kuburuga ekari 21,000 za kilimo cha mpunga Unguja na Pemba;

c) Kusimamia na kurahisisha upatikanaji na matumizi ya zana za kisasa za kilimo zitakazopelekea kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo;

d) Kutengeneza matrekta na zana zake na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi na vipuri kwa ajili ya huduma;

e) Kutoa mafunzo kwa madereva 60 (34 Unguja na 26 Pemba) na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wasimamizi wa huduma za matrekta mashambani

**83.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 2.16 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 787.60 milioni ni mshahara na TZS 1.37 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa Mwaka 2020/2021**

**84.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuwajengea uwezo wataalamu kutoka Halmashauri za Wilaya 11 Unguja na Pemba juu ya Uhakika wa Chakula na Lishe;

b) Kuendeleza na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya hali ya chakula na lishe katika ngazi zote Unguja na Pemba;

c) Kuandaa mafunzo ya maafisa wa Wilaya na Shehia na Kamati za Uhakika wa Chakula na Lishe;

d) Kuandaa mikutano ya Baraza la Uhakika wa Chakula na Lishe la Taifa;

e) Kuimarisha mashirikiano na taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa zinazohusiana na uhakika wa chakula na lishe.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS1.61 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 222.87 milioni Mshahara, TZS 458.50 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 931.69 kutoka kwa washirika wa maendeleo).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni:

a) Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu;

b) Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Maendeleo ya Misitu inaombewa jumla ya

**TZS 5.84 bilioni** ambapo **TZS. 2.04 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.68 bilioni ni mishahara na TZS 359.35 milioni matumizi mengineyo) na **TZS 3.80 bilioni** kwa Miradi ya Maendeleo kutoka UNDP.

**Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu kwa mwaka 2020/2021**

**88.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuotesha miche 1,800,000 (1,500,000 Misitu; 300,000 ya matunda na viungo) katika vitalu vya Serikali;

b) Kuhamasisha uekezaji na kutangaza vivutio vya utalii wa kimaumbile ndani na nje ya Zanzibar ili kufikia watalii 100,000;

c) Kufanya doria 200 katika maeneo ya maliasili za misitu kwa lengo la kudhibiti matukio ya uhalifu na uharibifu;

d) Kupandisha hadhi maeneo mawili ya misitu ya jamii (Mtambwe Pemba na Uzi-Vundwe Unguja) na kuwa misitu ya hifadhi;

e) Kufanya utafiti wa kujua idadi ya wanyama adimu na mazingira yao wakiwemo paa nunga, popo wa Pemba na Paa chesi wa Pemba.

f) Kuongeza uzalishaji wa asali kutoka tani 13.3 hadi 25 kwa kuwawezesha wazalishaji wakubwa 15 wa

nyuki (Pemba 10 na Unguja 5) juu ya uzalishaji wa kibiashara wa asali.

**89.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 135.09 milioni** kwa matumizi mengineyo na TZS. 3.80 bilioni kwa ajili ya kazi za Maendeleo kutoka UNDP.

**Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka 2020/2021**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuandaa na kutekeleza mpango wa urejeshaji wa maeneo yaliyochimbwa rasimalimali za kifusi, mawe na mchanga;

b) Kufanya utafiti wa kuangalia namna bora ya upatikanaji wa mchanga, mawe na kifusi nchini;

c) Kuandaa mfumo wa uwekaji wa taarifa za uchimbaji, usafirishaji na matumizi ya maliasili zisizorejesheka;

d) Kutoa taaluma ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka kupitia vipindi vya Radio, T.V, warsha na makongamano;

e) Kuendelea kutoa huduma za upatikanaji wa mchanga, mawe, kokoto na kifusi kwa wananchi, wawekezaji na miradi mikubwa ya maendeleo;

f) Kudhibiti uchimbaji na usafirishaji haramu wa

maliasili zisizorejesheka kwa kufanya doria 100 katika maeneo yote ya Unguja na Pemba

**91.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 1.91 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida (TZS 1.68 bilioni ni mishahara na TZS 224.26 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Mifugo ina jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

**Programu imegawika katika Programu Ndogo Mbili**

a) Programu ndogo ya uzalishaji mifugo

b) Programu ndogo ya huduma za utabibu wa mifugo

**93.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Maendeleo ya Mifugo inaombewa jumla ya **TZS 3.68 bilioni,** kati ya fedha hizo **TZS. 2.68 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.31 bilioni Mshahara, TZS 233.66 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS 1.14 bilioni ikiwa ni Ruzuku) na **TZS 1.00 bilioni** kutoka SMZ kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka 2020/2021

**94.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mifugo;

b) Kuimarisha malisho kwa kupanda majani ekari 10 katika eneo la Kizimbani;

c) Kuanzisha mpango wa uzalishaji wa ng'ombe chotara wa maziwa Pangeni;

d) Kuwaunganisha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika kiwanda cha Azam;

e) Kuwashajiisha wafugaji na madaktari wa mifugo vijijini (CAHW'S) katika uzalishaji wa mazao ya mifugo (maziwa, mayai na nyama).

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo inaombewa jumla ya **TZS 128.27** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo kwa Mwaka 2020/2021**

a) Kuchanja kuku 200,000 (Unguja 150,000 na 50,000 Pemba) dhidi ya ugonjwa wa Mahepe, Gumboro na Ndui;

b) Kuchanja ng'ombe 10,000 dhidi ya magonjwa chambavu (BQ), kimeta (anthrax), ugonjwa wa ngozi (LSD) na ugonjwa wa miguu na midomo (FMD);

c) Kuchanja mbwa 8,000 (5,000 Unguja na 3,000 Pemba) dhidi ya kichaa cha mbwa;

d) Kutoa huduma ya maabara ya mifugo;

e) Kuimarisha huduma za kinga na tiba;

f) Kufunga uzazi jumla ya mbwa na paka 200 ili kupunguza tatizo la wanyama wazururaji.

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inaombewa jumla ya **TZS 1.42 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.31 bilioni Mishahara na TZS 105.38 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo).

## Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo

**97.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI) inalenga kutekeleza shabaha zifuatao:

a) Kufanya tafiti 5 za mifugo zikiwemo; Tathmini ya Kuku wa Kienyeji, Tathmini ya Mbuzi wa Kienyeji, kutafiti ubora na usalama wa maziwa, utafiti wa aina ya kupe na madhara yao na kutathmini ubora wa vyakula vya mifugo;

b) Ukarabati wa miundombinu iliyopo Makao Makuu ya ZALIRI, Kizimbani Unguja na ujenzi wa jengo la ofisi pamoja na banda la kuwekea ng’ombe wa utafiti, Chamanangwe, Pemba;

c) Kujenga banda la kuweka wanyama wa maabara kwa madhumuni ya kuwafanyia utafiti;

d) Kufanya majaribio ya aina tatu za mwani ili kujua kiwango cha lishe kwa kila aina ya mwani na faida zake kwa wanyama;

e) Kuhudhuria mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, inaombewa jumla ya **TZS 2.14 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 519.60 milioni ni mshahara na TZS 623.30 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 1.0 bilioni fedha za Maendeleo kutoka SMZ).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 27.03 bilioni** kati ya hizo **TZS. 1.35 bilioni** kwa matumizi ya kawaida (TZS 769.02 milioni ni Mishahara, **TZS 306.81 milioni** ni matumizi mengineyo na TZS 272.00 milioni ni Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini) na **TZS 25.68 bilioni** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (**TZS 2.00 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 23.68 bilioni** kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

**Programu imegawika katika Programu Ndogo Mbili**

a) Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini

b) Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini**

**100. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2020/2021,

**Programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:**

a) Kuimarisha doria shirikishi 174 katika maeneo ya hifadhi Unguja na Pemba;

b) Kukamilisha ujenzi wa Chelezo katika eneo la Kampuni ya Uvuvi – ZAFICO;

c) Kukamilisha jengo la maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini;

d) Kuendelea na ujenzi wa Diko na Soko la Kisasa la Samaki linalojengwa Malindi;

e) Kuendeleza mashirikiano ya uvuvi na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika kuendeleza sekta ya uvuvi nchini.

f) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 8 ili kuimarisha taaluma za uvuvi;

**101. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ndogo hii inaombewa **TZS 25.86 bilioni** kati ya hizo TZS.922.43 milioni kwa kazi za kawaida (TZS 769.02 milioni ni mishahara, TZS 153.41 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo) na TZS. 24.94 kwa kazi za maendeleo (TZS 2.00 bilioni kutoka SMZ na TZS 22.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

**Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini**

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo hii:**

**102. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuzalisha vifaranga milioni 10 vya majongoo bahari, samaki na kaa;

b) Kutoa elimu kwa wafugaji 95 wa mazao ya baharini Unguja na Pemba;

c) Kuimarisha miundombinu ya ufugaji na kusambaza vifaranga vya kaa, samaki na majongoo bahari;

d) Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi 7 wa kituo cha kutotolea vifaranya vya samaki, kaa na majongoo bahari wa kituo cha Beit-al-Ras;

e) Kuendelea kuhamasisha wakulima wa zao la mwani kuongeza uzalishaji wa mwani wenye tija na usarifu wa bidhaa za mwani.

**103.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu hii ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini inaombewa **TZS 889.88 milioni** ambapo (TZS 153.40 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 736.48 kutoka kwa washirika wa maendeleo).

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini**

**104.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kukamilisha tafiti 1 inayoendelea kuhusiana na Kipato na Matumizi kwa Wavuvi wa Kienyeji na kufanya tafiti 4 mpya zinazohusiana na uvuvi na mazao ya baharini zikiwemo za mwani, majongoo bahari na samaki;

b) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya baharini;

c) Kuchapisha kitabu chenye taarifa za tafiti za uvuvi zilizofanywa Zanzibar kuanzia mwaka 2000 kuhusiana na uvuvi na mazao ya baharini kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi;

d) Kuajiri na kujenga uwezo watafiti na wataalamu watakaotoa huduma bora katika kutekeleza tafiti za uvuvi na za mazao ya baharini;

e) Kuendeleza mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya baharini;

f) Kufanya Utafiti wa aina mpya ya mwani wa Glacelaria katika maeneo ya Fumba na Nyamanzi.

**105. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inaombewa jumla ya **TZS 272.0 milioni** kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

**Kampuni ya Uvuvi**

**106. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) kwa mwaka wa fedha 2020/2021, inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuvua na kusambaza samaki tani 300 katika mahoteli ya kitalii na kampuni binafsi;

b) Kukamilisha ununuzi wa Boti ya Uvuvi ya pili;

c) Kujenga kiwanda cha usarifu wa madagaa;

d) Kuanza ujenzi wa kiwanda cha usarifu wa minofu ya samaki pamoja na miuondombinu ya baridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki pamoja na usimamizi wa ujenzi wa chelezo kwa ajili ya maegesho ya boti za ZAFICO;

e) Kujenga Shamba la ufugaji wa samaki baharini katika eneo la Mkokotoni Kaskazini Unguja;

f) Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 10 ili kuimarisha uwezo wao wa kazi kulingana na mahitaji ya Kampuni;

g) Kushajiisha jumuiya za wavuvi kuvua dagaa na samaki wa aina ya Jodari kwa ajili ya kusarifu na kusafirisha nje ya nchi.

107. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO inatarajia kuingiziwa **TZS 9.8 bilioni** ambapo **TZS 8.1 bilioni** kutoka kwa mashirika yenye hisa (ZSSF, ZSTC, ZIC na ZPC) na **TZS 1.7 bilioni** ikiwa ni pato litakalotokana na uzalishaji wake kwa kipindi hicho.

## PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA UTAWALA WA KAZI ZA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

108. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi wa sekta za kilimo.

**Programu imegawika katika program ndogo tatu nazo ni:**

a) Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi;

b) Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti;

c) Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi Pemba.

**109. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo inaombewa jumla ya **TZS 14.26 bilioni** kati ya hizo **TZS 6.45 bilioni** (TZS 5.30 bilioni ni mshahara, TZS 1.15 matumizi mengineyo) na TZS 7.81 kwa ajili ya kazi za maendeleo kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

**110. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta za kilimo, misitu, mifugo na uvuvi.

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji kwa Mwaka 2020/2021**

a) Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 1,200 na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi;

b) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma Wafanyakazi 51 wanaoendelea na masomo (PhD 1, MSc 1, B.Sc 48 na Diploma 1);

c) Udhibiti na ufuatiliaji wa mali za Serikali ikiwemo upimaji wa mashamba matatu (Kilombero, Pangeni na Wesha) na kuyapatia hatimiliki;

d) Kuendelea na ukaguzi wa mahesabu ya ndani pamoja na vikao vya zabuni kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa na huduma;

e) Kuendelea kutoa taarifa za sekta ya kilimo na maliasili kupitia vyombo vya habari, majarida kwa njia ya mtandao;

f) Kutoa mafunzo kwa wastaafu 50 watarajiwa.

111. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, inaombewa jumla ya **TZS 2.36 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.82 bilioni ni mishahara na TZS 542.63 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

112. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za mipango sera na utafiti kwa maendeleo ya sekta za kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2020/2021**

113. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuandaa, kupitia Sera, Kanuni na Mikakati (Sera ya usimamizi wa misitu, Sera na Sheria ya uvuvi, Sheria ya mbegu na Sheria ya utibabu na udhibiti wa mimea);

b) Kutayarisha Mipango Mikakati ya Kilimo ya Wilaya na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ZASDP;

c) Kufanya tafiti za kiuchumi na Kijamii kwa mujibu wa Zanzibar Research Agenda na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo;

d) Kuifanya kongamano la utafiti wa sekta ya kilimo;

e) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Takwimu;

f) Kuendeleza mashirikiano na taasisi za ndani, kikanda na kimataifa

114. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Mipango inaombewa jumla ya TZS 8.38 bilioni kati ya hizo TZS 570.85 milioni (TZS 258.85 milioni mishahara, TZS 312.00 milioni kwa matumizi mengineyo) na TZS 7.81 bilioni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Pemba**

115. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya sekta ya kilimo, maliaisli, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango ya Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

116. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a. Kuratibu vikao vinne na ziara za Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;

b. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;

c. Kufanya vikao vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana idara na taasisi mbali mbali mtambuka za sekta ya kilimo-Pemba;

d. Kuratibu ziara za wageni na viongozi wa Wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Wizara pamoja na kuhudhuria katika sherehe na kumbu kumbu za kitaifa Pemba;

e. Kuimarisha mashirikiano na taasisi nyenginezo (Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii).

**117. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu hii inaombewa kutumia jumla ya **TZS 3.52 bilioni** (TZS 3.22 bilioni mishahara na TZS 295.37 milioni ni matumizi mengineyo).

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **10.46 bilioni** kupitia vianzio vyake 12 viliopo Unguja na Pemba.

**119. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, inaomba

kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 129.86 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 23.32 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 11.47 bilioni Mishahara na **TZS 5.22 bilioni** matumizi mengineyo na **TZS 6.63 bilioni** RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo Wizara imetengewa **TZS 106.54 bilioni** (TZS 83.54 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 23.00 bilioni** kutoka SMZ.

**120. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika ya Maendeleo kwa kuipa kipaumbele Sekta ya Kilimo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya uchumi, kijamii na kuwa na uhakika wa chakula Nchini. kwa mwaka fedha 2020/2021 Bajeti ya Sekta ya Kilimo imeongezeka na kufikia **TZS 129.86 bilioni** kutoka **TZS 88.17 bilioni** ilizopangiwa mwaka wa fedha 2019/2020 hili ikiwa ni ongezeko la **asilimia 47.3** za Bajeti ya Wizara.

## SHUKURANI

**121. Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi zikiwemo Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara Kazi, Uwezeshaji, Wazee,

Wanawake na Watoto, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Fedha na Mipango. Wizara ya Afya, Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisi ZSTC, TAHA, UWAMWIMA, ZAIDI, COSTECH, TAFIRI, TALIRI, TPRI, Milele Foundation, Kilimo Trust, Wizara ya Kilimo (SMT), Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT), CARI, Wizara ya Maliasili na Utalii (SMT), Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT), Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania, Taasisi ya Sayansi za Bahari (UDSM), *"State Oceanic Administration"* (SOA) ya China, Heifer Project Tanzania, Zanchick, "ZAASO", "ZSPCA" na "WIOMSA". Vile vile nachukua fursa hii kwa kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza Kilimo, Mifugo na Uvuvi, zikiwemo Japan, China, India, Israel, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Oman na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo nchini. Vilevile nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, ICRAF, IFAD, UNDP, FAO, JICA,
UNICEF, WFP, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, *Rockfeller Foundation na Bill and Melinda Gates Foundation*, *GIZ*, "WAP", "WHO", Shirika la Mionzi la Ulimwengu (IAEA), Indian Ocean Rim, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC) na Umoja wa nchi za Ulaya - "EU"

**122.** **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wanakamati za hifadhi za maliasili kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mifugo na mazao ya

baharini. Pia Napenda kumshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu wake wawili, Afisa Mdhamini WKMMU, Wakurugenzi wa Maidara na Taasisi za Wizara hii pamoja na watumishi wote wa Wizara pasi na kuzisahau Halmashauri zote na wadau wote wa Sekta ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa Shabaha za Wizara kwa mwaka 2019/2020. Ni matarajio kwamba tutaendelea kushirikiana tena katika mwaka 2020/2021.


123. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Ulinzi na Usalama, Baraza la Biashara la Taifa, Majukwaa ya Vijana, Kamati za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu, Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

123. **Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wajumbe** nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

**MHE. MMANGA MJENGO MJAWIRI (MBM) WAZIRI, WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI ZANZIBAR**


# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho Nam. 1A: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula, Mboga na Matunda (Tani)




## Kiambatanisho Nam. 1B: Idadi ya Mifugo Iliyokaguliwa na Kuchinjwa





**Kiambatanisho Nam. 1C: Uzalishaji wa Mayai Kiwilaya**




86


### Kiambatanisho Nam. 1D: Uzalishaji wa Maziwa (Lita)






87


**Kiambatanisho Nam. 1E: Uzalishaji wa Samaki (Tani)**







88

## Kiambatanisho Nam. 1F: Usafirishaji wa Mazao Baharini (Tani)




## Kiambatanisho Nam. 1 G: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu ($m^3$)




**Kiambatanisho Nam. 1H: Uzalishaji wa Mazao ya Maliasili Zisizorejesheka (Tani)**





**Kiambatanisho Nam. 2A: Makadirio ya Fedha za Kazi za Kawaida kwa Mwaka 2020/21**





## Kiambatanisho Nam. 2B: Jadweli la Upatikanaji wa Mapato Julai 2019 hadi Machi, 2020

| Kasma | Maelezo | Makadirio ya Mapato 2019/20 | Mapato halisi Julai hadi Machi 2019/20 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | | | | |
| 1422022 | Ada Ya Mazao Ya Misitu | 79,000,000 | 22,255,150 | 28 |
| 1422023 | Ada Ya Uuzaji Wa Mawe Na Michanga Na Kokoto | 788,448,000 | 578,962,385 | 73 |
| 1421001 | Mauzo Ya Uzalishaji Wa Miche | 38,500,000 | 661,000 | 2 |
| 1422060 | Mapato Ya Mashamba | 206,000,000 | 516,566,300 | 251 |
| 1422066 | Ada Ya Uingizaji Wa Wageni | 13,000,000 | 0 | 0 |
| 1422048 | Ada Ukaguzi Wa Mazao | 22,800,000 | 15,340,000 | 67 |
| 1422026 | Leseni Za Uvuvi | 21,900,000 | 10,563,100 | 48 |
| 1422027 | Ada Mazao Baharini | 12,377,000 | 22,564,140 | 182 |
| 1421011 | Utibabu Wa Wanyama | 42,500,000 | 9,488,450 | 22 |
| 1422068 | Mapato Ya Mifugo | 18,000,000 | 228,000 | 1 |
| | **Jumla Ndogo Pemba** | **1,242,525,000** | **1,176,628,525** | **95** |
| **Idara Ya Misitu Na Maliasili Zisizorejesheka** | | | | |
| 1422022 | Ada Ya Mazao Ya Misitu | 207,129,600 | 331,451,341 | 160 |
| 1422023 | Ada Ya Uuzaji Wa Mawe Na Michanga Na Kokoto | 6,904,076,000 | 3,596,330,091 | 52 |
| 1421001 | Mauzo Ya Uzalishaji Wa Miche | 11,160,000 | 2,038,600 | 18 |
| | | | 521,500 | |
| | **Jumla Ndogo** | **7,122,365,600** | **3,930,341,532** | **55** |
| **Idara Ya Kilimo** | | | | |
| 1422048 | Ada Ukaguzi Wa Mazao | 55,800,000 | 77,593,785 | 139 |
| | **Jumla Ndogo** | **55,800,000** | **77,593,785** | **139** |
| **Taasisi Ya Utafiti Wa Kilimo** | | | | |
| 1423002 | Mauzaji Ya Mazao Na Miche | 52,080,000 | 8,489,000 | 16 |
| 1422060 | Mapato Ya Mashamba | 14,880,000 | 56,259,000 | 378 |
| 1422066 | Ada Ya Uingizaji Wageni | 37,200,000 | 17,181,000 | 46 |
| | **Jumla Ndogo** | **104,160,000** | **81,929,000** | **79** |


93

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Idara Ya Uvuvi** | | | | |
| 1422026 | Leseni Za Uvuvi | 116,250,000 | 34,536,200 | 30 |
| 1422067 | Mapato Ya Uvuvi Wa Bahari Kuu | 1,526,080,000 | 0 | 0 |
| 1422027 | Ada Mazao Baharini | 234,800,000 | 344,273,947 | 147 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,877,130,000** | **378,810,147** | **20** |
| **Idara Ya Mifugo** | | | | |
| 1421011 | Utibabu Wa Wanyama | 52,080,000 | 79,662,200 | 153 |
| 1422068 | Mapato Ya Mifugo | 14,203,400 | 930,500 | 7 |
| | **Jumla Ndogo** | **66,283,400** | **80,592,700** | **122** |
| | **Jumla Ndogo Unguja** | **9,225,739,000** | **4,549,267,164** | **49** |
| | **Jumla Unguja Na Pemba** | **10,468,264,000** | **5,725,895,689** | **55** |



94

## Kiambatanisho Nam. 2C: Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2019 - Machi 2020

| **Program Kuu/Program Ndogo** | **Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Machi 2020** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mshahara** | **Matumizi Kawaida** | **Ruzuku Kawaida** | **Ruzuku Mshahara** | **Maendeleo SMZ** | **Maendeleo Mhisani** | **JumlA** |
| **PL0101 Maendeleo ya Kilimo** | **1,734,536,080** | **2,979,527,889** | **1,000,838,666** | **2,233,009,022** | **704,000,000** | **4,936,742,116** | **13,588,653,773** |
| SL010101 Umwagiliaji maji | 333,565,500 | 103,148,249 | - | - | 704,000,000 | 4,936,742,116 | 6,077,455,865 |
| SL010102 Utafiti na Mafunzo ya kilimo-ZARI | - | - | 414,599,109 | 1,654,812,860 | - | | 2,069,411,969 |
| SL010103 Maendeleo ya huduma za kilimo | 1,208,425,880 | 2,603,116,460 | - | - | - | | 3,811,542,340 |
| SL010104 Uhakika wa chakula na lishe | 192,544,700 | 273,263,180 | - | - | - | | 465,807,880 |
| SL010105 Karakana ya Matrekta | - | - | 586,239,557 | 578,196,162 | - | | 1,164,435,719 |
| **PL0102 Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka** | **1,469,037,325** | **214,536,211** | **-** | **-** | **579,400,000** | **72,000,000** | **2,334,973,536** |
| SL010201 Maendeleo na Uhifadhi wa misitu | - | 111,316,822 | - | - | - | 72,000,000 | 183,316,822 |
| SL010202 Usimamizi wa Maliasili zisizorejesheka | 1,469,037,325 | 103,219,389 | - | - | 579,400,000 | | 2,151,656,714 |
| **PL0103 Maendeleo ya Mifugo** | **962,430,340** | **101,048,125** | **383,472,129** | **305,700,000** | **-** | **-** | **1,752,650,594** |
| SL010301 Uzalishaji wa mifugo | - | 41,330,858 | - | - | - | | 41,330,858 |
| SL010302 Huduma za utabibu wa mifugo | 962,430,340 | 59,717,267 | - | - | - | | 1,022,147,607 |


95

96

| Program Kuu/Program Ndogo | Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Machi 2020 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mshahara | Matumizi Kawaida | Ruzuku Kawaida | Ruzuku Mshahara | Maendeleo SMZ | Maendeleo Mhisani | JumlA |
| SL010303 Taasisi ya Utafiti wa mifugo | - | - | 383,472,129 | 305,700,000 | - | | 689,172,129 |
| **PL0104 Maendeleo ya Uvuvi** | **559,580,025** | **141,208,926** | **188,000,000** | **-** | **1,400,000,000** | **13,334,803,179** | **15,623,592,130** |
| SL010401 Kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini | - | 69,181,821 | - | - | - | - | 69,181,821 |
| SL010402 Maendeleo ya uvuvi na hifadhi za baharini | 559,580,025 | 72,027,105 | - | - | 1,400,000,000 | 13,334,803,179 | 15,366,410,309 |
| SL010402 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini | - | - | 188,000,000 | - | - | | 188,000,000 |
| **PL0105 Mipango na Usimamizi wa Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvi** | **3,825,153,185** | **1,175,595,735** | **-** | **-** | **554,000,000** | **5,655,261,569** | **11,210,010,489** |
| SL010501 Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili mifugo na uvuvi | 1,195,078,860 | 690,417,375 | - | - | - | | 1,885,496,235 |
| SL010502 Mipango, sera na utafiti wa kilimo maliasili mifugo na uvuvi | 214,815,390 | 200,998,218 | - | - | 554,000,000 | 5,655,261,569 | 6,625,075,177 |
| SL010503 Uratibu Ofisi kuu Pemba | 2,415,258,935 | 284,180,142 | - | - | - | | 2,699,439,077 |
| **Jumla Kuu** | **8,550,736,955** | **4,611,916,886** | **1,572,310,795** | **2,538,709,022** | **3,237,400,000** | **23,998,806,864** | **44,509,880,522** |

**Kiambatanisho Nam. 2D: Jadweli la Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Julai 2019 hadi Machi 2020**

| MRADI | MAKISIO 2019/2020 | | | FEDHA ZILOPATIKANA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | SMZ | MUHISANI | JUMLA | SMZ | MUHISANI | JUMLA |
| Mradi wa umwagiliaji maji -KOREA | 1,000,000,000 | 32,867,000,000 | 33,867,000,000 | 704,000,000 | 4,936,742,116 | 5,640,742,116 |
| Mradi wa Miundombinu ya Sekta ya Kilimo-SMZ | 1000,000,000 | - | 1,000,000,000 | 518,000,000 | - | 518,000,000 |
| Programu ya kuendeleza utafiti wa sekta ya Mifug - SMZ | 1,200,000,000 | - | 1,200,000,000 | - | - | - |
| Mradi wa Uimarishaji mazao ya baharini – FAO | 200,000,000 | 692,423,000 | 892,423,000 | - | 2,607,077,000 | 2,607,077,000 |
| Mradi wa Usimamizi Uvuvi Bahari Kuu - SWIOFish | 50,000,000 | 2,894,693,000 | 2,944,693,000 | - | 3,798,696,179 | 3,798,696,179 |
| Ujenzi wa Soko la Malindi | 1,400,000,000 | 13,200,000,000 | 14,600,000,000 | 1,400,000,000 | 6,929,030,000 | 8,329,030,000 |
| MIVARF | - | 399,616,000 | 399,616,000 | - | 275,272,050 | 275,272,050 |


97

| MRADI | MAKISIO 2019/2020 | | | FEDHA ZILOPATIKANA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | SMZ | MUHISANI | JUMLA | SMZ | MUHISANI | JUMLA |
| ERPP | 80,000,000 | 6,950,283,000 | 7,030,283,000 | 36,000,000 | 5,245,398,841 | 5,281,398,841 |
| Safeguarding Zanzibar Forest And Coastal Habitats For Multiple Ben | | 228,200,000 | 228,200,000 | | | |
| Food Climate Resilient Project | | 44,400,000 | 44,400,000 | | | |
| Tanzania Initiative For Preventing Aflatoxin Contamination (Tanipac) | | 988,440,000 | 988,440,000 | - | 134,590,678 | 134,590,678 |
| Agri-Connect-Supporting Value Chains For Shared Prosperity | | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | | | |
| Forest Development Fund | | | | 579,000,000 | 72,000,000 | 579,000,000 |
| **Jumla** | **4,930,000,000** | **60,265,055,000** | **65,195,055,000** | **3,237,000,000** | **23,935,548,980** | **27,235,806,864** |


98

99

## Kiambatanisho Nam. 3: Idadi ya Tafiti za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

| NAM. | UTAFITI | LENGO | ENEO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| **A. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi** | | | | |
| 1. | Kufanya utafiti wa survey ya biashara zinazohusiana na mambo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini” | Kujua vikundi/ wajasiriamali wa sekta ya uvuvi katika maeneo husika. | Maeneo ya Wilaya zinazojishughulisha na uvuvi wa maji chumvi kwa Tanzania Bara na Visiwani. | Utafiti umekamilika |
| 2. | Utafiti wa kuangalia usambaaji wa pweza na nguvu inayotumika kuwavua na uwezekano wa kufunga mazalia ya pweza Zanzibar. | Kuangalia uwezo wa kuongeza uzalishaji na usimamizi madhubuti wa rasilimali ya pweza. | Maeneo yaliyochaguliwa ndani ya Hifadhi za Baharini za Unguja na Pemba. | Utafiti umekamilika |
| 3. | Tathmini ya matumbawe katika Bahari ya Magharibi ya Kisiwa cha Unguja kwa kutumia kifaa cha kupigia picha chini ya bahari.***“Sona and video*** | Kujua hali halisi ya matumbawe katika bahari ya magharibi ya kisiwa cha unguja | Unguja | Utafiti umekamilika |

| NAM. | UTAFITI | LENGO | ENEO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| | ***method"*** | | | |
| 4. | Utafiti wa aina nne za mwani aina ya *Agar glacilaria* zinazopatikana Zanzibar | Kuweza kujua mbinu za uzalishaji pamoja na thamani kwa ajili ya kuengeza tija. | Unguja na Pemba | Utafiti unaendelea |
| 5. | Utafiti wa hali ya uvuvi wa pweza, upatikanaji na mfumo wa ufungaji wa maeneo ya uvuvi wa pweza | Kutathmini hali ya uvuvi wa pweza, upatikanaji na mfumo wa ufungaji wa maeneo ya uvuvi wa pweza | Uroa na Kizimkazi Mkunguni Unguja | Utafiti upo katika hatua ya mwisho |
| 6. | Taarifa za awali za hali halisi ya uvuvi katika maeneo ya matumbawe unaofanyika maeneo ya hifadhi ya bahari ya Zanzibar | Kufanya tathmini ya hali ya uvuvi katika maeneo yaliyochaguliwa ya matumbawe, ikijumuisha tathmini ya uzalishaji kwa kiwango na aina ya samaki | Hifadhi ya Ghuba ya Menai, Hifadhi ya Maeneo ya Kisiwa cha Mnemba (MICA) na Hifadhi ya Maeneo ya Bahari ya Pemba (PECCA) | Utafiti huu unafanywa kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) |
| 7. | Utafiti wa Uvuvi wa Pweza Zanzibar | Kutafiti kiwango cha pweza na mgawanyiko | Unguja Ukuu na Uroa (Unguja) na Mkoani, , | Utafiti huu unafanywa kwa |

100

| NAM. | UTAFITI | LENGO | ENEO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| | | wa uvuvi wa pweza Zanzibar | Chake na Wete Pemba | kushirikiana na SUZA |
| 8. | Utafiti wa Uvuvi wa Samaki Jamii ya Dagaa Zanzibar | Kufanya uchambuzi wa uvuvi wa samaki jamii ya dagaa ili kujua aina na kiwango chake Zanzibar | Unguja na Pemba | Utafiti huu unafanywa kwa kushirikiana na SUZA |
| 9. | Utafiti wa kiwango, aina na mgawanyiko wa samaki jamii ya jodari katika mwambao wa bahari ya Zanzibar | Kufanya uchambuzi wa kijamii na kiuchumi, fursa na changamoto zinazohusiana na uvuvi wa samaki wa Jamii ya Jodari | Kizimkazi Mkunguni, Kizimkazi Dimbani, Mtende, Unguja UKuu (Menai), Nungwi, Fukuchani, Potoa, Matemwe, Chwaka na Uroa (Unguja) na Wete na Mkoani (Pemba) | Utafiti huu unafanywa kwa kushirikiana na SUZA |
| 10. | Kufanya utafiti wa kujua maeneo bora ambayo yanaweza kufugika majongoo bahari Zanzibar | Kufanya utafiti wa kuelewa maeneo bora ya kufuga majongoo bahari ili kuwasaidia jamii | Vijiji 15 Unguja na Vijiji 10 Pemba | Utafiti huu umekamilika |

| NAM. | UTAFITI | LENGO | ENEO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| | | kuifanya shughuli hii ipasavyo | | |
| 11. | Taarifa za tafiti za Uvuvi na Mazao ya Baharini zilizofanywa katika maeneo ya Unguja na Pemba | Kukusanya taarifa za tafiti za Uvuvi na Mazao ya Baharini zilizofanywa katika maeneo ya Unguja na Pemba | Unguja na Pemba | Utafiti huu umekamilika |
| 12. | Kufanya utafiti wa hali ya uchumi jamii kwa wavuvi wa kienyeji; | Kujua kipato na matumizi cha wavuvi ili kuweza kujua mbinu za kutumia kuwasaidia na kukuza kipato chao | Madiko 20 ya Unguja na madiko 11 ya Pemba | Utafiti unaendelea |
| **B. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI** | | | | |
| 1. | Kutengeneza mbegu za mpunga zenye kuvumilia maradhi ya ukungu kwa kutumia teknologia ya mionzi. | Lengo ni kutoa mbegu mpunga zitakozovumilia maradhi ya ukungu | Kizimbani na Uzini | Utafiti unaendelea |
| 2. | Uchunguzi wa mbegu za mpunga zitakazohimili mazingira ya Zanzibar na zenye | Kuibua mbegu ya mpunga miongoni mwa mbegu zilizoingizwa | Unguja na Pemba | Utafiti unaendelea |



102

| NAM. | UTAFITI | LENGO | ENEO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| | sifa za ulaji zinazokubalika Zanzibar | kutoka nje ya nchi ambayo itakubaliana na mazingira ya Zanzibar | | |
| 3. | Kufanya makusanyo ya vinasaba vya mbegu za mpunga za kienyeji na za kigeni. | Kuangalia na kuhifadhi mbegu za kienyeji na nje zilizopo Zanzibar kwa matumizi ya baadae | Kizimbani Unguja | Utafiti unaendelea |
| 4 | Kufanya makusanyo ya vinasaba ya mbegu za migomba za kienyeji na za kigeni. | Kukusanya na kufanya uchunguzi wa aina ya migomba yenye uwezo wa kustahamili maradhi ya ***Sigatoka, Panama*** | Kizimbani Unguja na Matangatuani Pemba | Kazi hii itaendelea. |
| 5. | Athari ya kukata vilele katika mavuno na ubora wa matikiti maji | Kuchunguza kiwango cha mavuno ya matikiti maji baada ya kukata vilele. | Kizimbani | Ufiti unaendelea |
| 6. | Uchunguzi wa mbolea za asili na viwandani katika ubora wa zao la Pilipili boga. | Kupata aina ya mbolea itakayotumika kwa uzalishaji mkubwa wa pilipili boga | Kizimbani | Utafiti unaendelea |


103

104


| NAM. | UTAFITI | LENGO | ENEO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Uchunguzi wa masafa ya upandaji katika kuongeza mavuno ya zao la kunde. | Kupata masafa bora ya upandaji wa zao la kunde litakaloweza kuongeza mazao katika eneo | Kizimbani Unguja | Utafiti unaendelea |
| 8. | Uchunguzi wa mbegu za mtama zitakazohimili mazingira ya Zanzibar na zenye sifa za ulaji zinazokubalika Zanzibar | Kuibua mbegu mpya ya mtama itakayotumika katika maeneo ya ukanda wa juu ya muda mfupi | Unguja na Pemba | Utafiti utaendelea |
